
Nipashe
Ijumaa Mei 26, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581322
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



# MORRISON, GADIEL WATAJWA KUJIUNGA SINGIDA BIG STARS

UKURASA 20

SUPA JACKPOT
TZS. 1,117,417,539
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



## DC Korogwe azindua mbio za wajawazito

UKURASA 3



# Mwendo wa mageuzi Ardhi

UKURASA 2

- Mikopo kwa wananchi kujenga nyumba, watumishi kukopeshwa
- Utatuzi migogoro ya ardhi wawekewa mikakati
- Maeneo ya uwekezaji, miradi mikubwa, fidia kwa wananchi
- Mipaka kimataifa kumulikwa, wanafunzi 2,000 kudahiliwa, watendaji waovu watumbuliwa
- Mradi wa Nyumba za Samia wapewa kipaumbele
- Ajira mpya, waliopo kupandishwa vyeo

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula akiwasilisha makadirio ya bajeti ya wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wahitimu wote kidato cha sita kuchukuliwa mafunzo ya JKT

UKURASA 3

# Museveni ataka wawekezaji Tanzania kuuza gesi Uganda

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Rais wa Uganda, Yoweri Kaguta Museveni wakati alipotembelea mradi wa kufua umeme wa Kikagati – Murongo (Megawatt 16), baada ya kuuzindua, Mbarara nchini Uganda jana. Mradi huo, utanufaisha nchi zote mbili katika masuala ya nishati ya umeme. **PICHA: IKULU**

MICHEZO YANGA HATARI ZAIDI NDANI YA BOKSI CAF UK.24 MAONI, KATUNI UK.6




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, ACP Allan Bukumbi akionyesha meno makubwa ya tembo manne na vipande 7 kwa waandishi wa habari jana, waliyomkamata nayo Tony Vitus (48) mkazi wa Mbinga, mkoani Ruvuma, kwa kushirikiana na jeshi la uhifadhi, akiwa amebeba kwenye pikipiki yenye namba za usajili MC 413 ALH aina ya San LG, mkoani humo. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Ni mwendo wa mageuzi Ardhi

**Na Romana Mallya,** DODOMA

UKIISOMA au kuisikia mikakati ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka ujao wa fedha, utakubaliana na hoja kwamba kutashuhudiwa mageuzi makubwa katika sekta inazozisimamia.

Mbali na mambo mengine, wizara hiyo imepanga kukamilisha miradi mikubwa iliyosimama ya Kawe 711 na Golden Premium Residence mkoani Dar es Salaam na kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Samia Housing Scheme (SHS) wa ujenzi wa nyumba 560 katika eneo la Kawe.

Pia imepanga kuendelea kutatua migogoro ya ardhi ambayo ndio kilio kikubwa cha wananchi katika maeneo mengi nchini huku ikitarajia kupata vibali vya kutoa ajira mpya 76, kupandisha vyeo 346 na kubadilishwa kada watumishi 15.

Waziri wake, Dk. Angelina Mabula, alitangaza mikakati hiyo jana bungeni jijini hapa alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24. Aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 171.372 kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati hiyo.

**MIRADI MIKUBWA**

Waziri Mabula alisema serikali ilitoa rukhsa kwa Shirika la Nyumba Tanzania (NHC) kukopa Sh. bilioni 173.9. Hadi sasa limekopa Sh. bilioni 44.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Morocco Square, Kawe 711, Golden Premier Residence na PLOT 300 Regent Estate.

"Hadi kufikia Mei 15 mwaka huu, mradi wa Morocco Square umekamilika kwa asilimia 100; miradi ya Kawe 711 na Golden Premier Residence mazungumzo kati ya Shirika na makandarasi yanaendelea ili kazi iendelee.

"Na mradi wa PLOT 300 Regent Estate haukutekelezwa kutokana na fedha iliyokuwa imetengwa kuhamishiwa katika mradi wa nyumba 5,000 za gharama nafuu wa Samia Housing Scheme zitakazojengwa kwa awamu katika mikoa mbalimbali kwa gharama ya Sh. bilioni 466. Kwa kuanzia, shirika lilianzia na nyumba 560 Kawe na utekelezaji umefikia asilimia 15 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2023/24," alisema.

Waziri huyo pia alisema shirika litaendelea na ujenzi wa nyumba 500 katika Jiji la Dodoma maeneo ya Njedengwa, Iyumbu na Medeli; ujenzi wa majengo ya biashara katika miji mbalimbali ikiwamo Bukoba, Tabora, Dodoma, Iringa, Kahama, Morogoro, Masasi na Lindi.

Pia alisema wanaendelea kutekeleza Sera ya Ubia kwa kuishirikisha sekta binafsi katika uwekezaji na uendelezaji wa majengo ya biashara na makazi na kuendelea kutekeleza mpango wa miaka mitano wa ukarabati wa nyumba za shirika (2022-2027).

"Pia tunaendelea na utekelezaji wa miradi ya ukandarasi ikiwamo ujenzi wa majengo ya ofisi za wizara nane jijini Dodoma, ujenzi wa jengo la Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ujenzi wa majengo manne ya Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA), ujenzi wa jengo la Kituo cha Biashara ya Madini ya Tanzanite Mirerani na ujenzi wa jengo la Kitengo cha Moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

**MIGOGORO ARDHI**

Waziri Mabula alisema kuwa katika mwaka 2023/24, wizara itaendelea kuimarisha uratibu na usimamizi wa maendeleo ya sekta ya ardhi kwa kuwekeza zaidi katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji huduma na upatikanaji wa taarifa za ardhi, kuweka mazingira rafiki ya upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji na kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi.

"Serikali itaendelea na utaratibu wa kutatua migogoro katika mikoa yenye migogoro mingi ikiwamo Arusha, Mwanza, Mbeya na Morogoro. Wizara itafungua mabaraza mapya 47 na kushughulikia mashauri 33,250," alisema.

Waziri alisema wizara itaratibu na kusimamia uandaaji wa taarifa za udhamini 54,000. Kati yake, uthamini wa kawaida 20,000 na udhamini wenye wafidiwa 34,000.

**MATUMIZI ARDHI**

Waziri Mabula alisema katika mwaka 2023/24, wizara kupitia Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi itaendelea kuandaa, kuwezesha, kuratibu na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya tano na vijiji 410 ambapo mipango ya wilaya tano na vijiji 210 itaandaliwa kupitia fedha za ndani za maendeleo na mipango ya vijiji 200 itaandaliwa kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP).

"Pamoja na jitihada za wizara kupitia tume katika utekelezaji wa jukumu hili, ninatoa rai kwa halmashauri za wilaya kutoa kipaumbele katika kutenga fedha za uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi," aliagiza.

Waziri Mabula alisema jumla ya mipangokina 14 ya vitovu vya vijiji na mashamba imeandaliwa katika halmashauri za wilaya ambayo imewezesha uwekaji wa miundombinu na huduma za jamii, utoaji wa hati za hakimilki za kimila 7,515 katika vijiji vinane vya halmashauri.

Akivitaja kuwa ni Nzega (Buduba na Seki), Kondoa (Haubi na Mafai), Mkalama (Munguli), Handeni (Msomera) na Chalinze katika vijiji vya Pongwe Mnazi na Pongwe. Wizara itaendelea na kazi hii mwaka ujao wa fedha.

Alisema wizara kupitia tume hiyo, itaendelea kuziwezesha mamlaka za upangaji na kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria za ardhi, miongozo na taratibu za upangaji, usimamizi na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

"Wizara kupitia tume itafanya utafiti katika maeneo mawili yanayohusu matumizi ya ardhi na maendeleo ya vijiji katika halmashauri mbalimbali na kusambaza matokeo kwa wadau, kuendelea kuhifadhi katika mfumo taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 810 na wilaya 10.

Dk. Mabula alisema wizara inatarajia kupata vibali vya ajira mpya 76, kupandisha vyeo 346 na kubadilishwa kada watumishi 15.

Alisema wizara itaandaa na kutoa hatimiliki za kimila 520,000, hatimiliki 500,000 na hati za sehemu ya jengo 1,000 na kuendelea kuratibu ugawaji na usimamizi wa maeneo ya ardhi ya uwekezaji.

Pia alisema wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 na kuendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali za sekta ya ardhi kwa lengo la kuziboresha.

Alisema kazi ya kuchakata taarifa zilizotokana na matokeo ya sensa ngazi ya taifa imekamilika na kubainisha Tanzania Bara ina majengo 13,907,951. Kati yake, 4,132,438 sawa na asilimia 29.7 yako mjini na 9,775,513 sawa na asilimia 70.3 yako vijijini.

## Museveni aomba wawekezaji Tanzania kuuza gesi Uganda

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, amesema nchi yake inaitegemea Tanzania kama mkombozi katika kuwapatia gesi kwa ajili ya kuendeshea baadhi ya shughuli za kiuchumi, ikiwamo kutengeneza chuma na kupikia.

Museveni alisema hayo jana nchini Uganda wakati wa hafla ya uzinduzi wa mradi wa kufua umeme wa Kikagati- Murongo wa megawati 16, iliyohudhuriwa pia na Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Rais Museveni alisema gesi iliyoko nchini mwake haitoshi na kwamba wanahitaji gesi nyingine kutoka Tanzania kwa ajili ya uzalishaji wa chuma, mbolea pamoja na kupikia.

"Tunategemea wenzetu Watanzania kutukomboa kutoka kwenye ukosefu wa gesi. Waganda sisi tuna kila kitu lakini hatuna gesi ya kutosha. Tena tunahitaji gesi ya chuma cha pua, tunataka gesi tutengeneze chuma, kwa ajili ya mbolea na kupikia.

"Kwa hiyo tunangojea kutoka Tanzania. Sisi tumewapelekea mafuta na wao watuletee gesi na huo ndio udugu wa daima," alisema Museveni.

Wakati wa hafla hiyo, Rais Samia alisema mradi huo wa kufua umeme utaimarisha ushirikiano na uhusiano baina ya nchi hizo mbili.

Pia alisema utaimarisha zaidi katika eneo la biashara na uwekezaji, uchumi wa nchi hizo mbili pamoja na usafiri na usafirishaji na kuboresha huduma za kijamii.

"Nchi zetu zinazidi kuandika historia ya ukuaji wa uchumi wake, jukumu letu kubwa ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwekeza katika eneo hili kwa sababu ndilo litaharakisha kujenga uchumi imara.

"Nishati ya umeme inayotengenezwa hapa, itainua mambo mengi ikiwamo eneo la mawasiliano, elimu, maji na usalama katika maeneo ya mijini na vijijini kwa sababu nishati itakuwapo ya kutosha," alisema.

Rais Samia alisema serikali ya Tanzania itaendelea kuweka nguvu zaidi na kuipa kipaumbele miradi yote ambayo inashirikiana na Uganda na kutaka timu za kusimamia miradi hiyo kutoka katika nchi hizo ziweke nguvu kuhakikisha inafanya kazi kama ilivyopangwa.

"Serikali ya Tanzania iko tayari kuendelea kuweka nguvu zaidi na kuipa kipaumbele miradi yote inayoshirikiana na Uganda na ninaamini hata wenzetu wako tayari katika hilo ili kuhakikisha inafanya kazi kama ilivyopangwa," alisema.

Mradi huo unaotokana na maji ya Mto Kagera, umegharimu Dola za Marekani milioni 56 na umezinduliwa Isingiro nchini Uganda.

# Wahitimu wote kidato cha 6 kuchukuliwa mafunzo JKT

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), limetangaza kuchukua wanafunzi wote waliohitimu kidato cha sita mwaka 2023 wa shule za Tanzania Bara kujiunga na mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria baada ya kuboresha miundombinu ya kambi zake.

Mkuu wa Tawi la Utawala wa JKT, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika makao makuu ya jeshi hilo kuhusu maandalizi ya mafunzo hayo.

Brigedia Mabena alisema wanafunzi hao wanatakiwa kuripoti kuanzia Juni Mosi hadi 11, mwaka huu katika kambi ambazo wamepangiwa kuripoti ili kuendelea na mafunzo.

"JKT tunazidi kuboresha miundombinu yetu kila iitwapo leo, tulianza kuchukua idadi ndogo, lakini hivi sasa tunachukua wanafunzi wote wanaohitimu kidato cha sita kwa mujibu wa sheria," alisema Brigedia Jenerali Mabena.

Brigedia Jenerali Mabena, alitaja makambi ambayo wanafunzi hao wanatakiwa kuripoti ni pamoja na JKT Rwamkoma (Mara), JKT Msange -(Tabora), JKT Ruvu (Pwani), JKT Mpwapwa, Makutupora JKT (Dodoma), JKT Mafinga (Iringa) na JKT Mlale (Ruvuma). Kambi nyingine ambazo wanafunzi hao wanatakiwa kuripoti ni JKT Mgambo, JKT Maramba (Tanga), JKT Makuyuni, Orjolo JKT (Arusha), JKT Bulombora, JKT Kanembe na JKT Mtabila (Kigoma), JKT Itaka (Songwe), JKT Luwa, Milundikwa (Rukwa), JKT Nachingwea (Lindi) JKT Kibiti (PWANI).

Alifafanua zaidi ya kuwa wahitimu wenye ulemavu wa kuonekana kwa macho (Physical Disabilities), wanapaswa kuripoti katika kambi ya JKT Ruvu iliyopo mkoani Pwani ambayo ina miundombinu yote ya kuhudumia watu wa jamii hiyo.

Alisema tayari imewasiliana na Wizara ya Elimu kwa ajili ya wanafunzi hao wa kidato cha sita waliohitimu mwaka huu kujiunga na mafunzo hayo.

Aidha, aliwataka vijana hao kuripoti kambini wakiwa na vifaa vyote ambavyo wanatakiwa kuwa navyo kama vilivyoanishwa zikiwamo nguo za kuzuia baridi kwa wale waliopangiwa mikoa yenye baridi.

"Safari hii taratibu zimerahisishwa unaingia katika mtandao unakuta kila kitu kimeanishwa kwa ajili ya maandalizi ya mafunzo hayo kwa vijana wa kwa mujibu wa sheria," alisema Brigedia Mabena.

Alisema udahili wa wanafunzi hao wa kidato cha sita wanaojiunga kwa mujibu wa sheria umepangwa kufanyika katika kambi ambazo watapangiwa huku akisisitiza orodha kamili ya vijana na makambi waliopangiwa inapatikana katika tovuti ya jeshi hilo.

Alifafanua mafunzo hayo ni muhimu kwa vijana hao kwa sababu yanawasaidia kuwajenga ikiwamo kujifunza stadi za kazi, nidhamu pamoja na weledi katika utendaji kazi wao pale wanapokuwa uraiani.




Msemaji Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, Gerson Msigwa akizungumza katika maadhimisho ya miaka 30 ya kuanzishwa kwa Taasisi ya vyombo vya habari Kusini mwa Jangwa la Sahara Tawi la Tanzania (Misa-Tanzania), jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Misa-Tan, Salome Kitomari. **PICHA: MARCO MADUHU**

# DC Korogwe azindua mbio za wajawazito

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa KOROGWE**

MKUU wa Wilaya ya Korogwe, Joketi Mwegelo, amezindua rasmi mbio za wajawazito zitakazofanyika Mei 28, mwaka huu kwa lengo la kuokoa afya zao.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mbio hizo, alisema zinaitwa 'Mamathon' yenye kaulimbiu ya Mwendo wa Mama, zitakazoanza ofisini kwake kuelekea viwanja vya Shule ya Msingi ya Mazoezi.

Alisema Mamathon itakuwa ni ya aina yake kufanyika na lengo lao ni kuwahamasisha kinamama na kuondoa dhana potofu wanazozipata wanapokuwa na ujauzito.

"Nadhani wengi hamjawahi kuona wanawake wajawazito wakikimbia sasa mtawaona Mei 28, mwaka huu, tuna jambo letu mapema," alisema.

Alisema kwa kutambua mwendo wa Rais Samia Suluhu Hassan, katika kuwaletea maendeleo wameona kama viongozi kuwa na wajibu wa kuwakutanisha jamii na kuyaenzi yale serikali yanayofanya.

Alisema kaulimbiu hiyo inatafsiri nyingi ambayo ni ule mwendo ambao ameuanza Rais Samia kwa namna anavyowaongoza katika nchi kuwa na maendeleo.

"Hii kaulimbiu yetu ya mwendo wa mama ni kutambua mchango wa Rais Samia jinsi anavyoitumikia Tanzania hususani alivyoligusa kundi la kinamama kwenye kila pembe na kila kona ya nchi," alisema. Alisema katika mbio hizo watatoa elimu ya afya ya uzazi na lishe kuhakikisha mama na mtoto wanakuwa afya njema.

"Hiyo siku tutazindua lishe bora ili tunapokuwa na lishe bora vizazi vyetu vinavyozaliwa vitakuwa na lishe nzuri na akili timamu na kujenga uchumi wa nchi hii pia ni ajenda ya Rais Samia," alisema. Mwegelo alisema mbio hizo pia zinawahusu wanawake wote, ni muhimu kujiandikisha katika vituo vya afya na hospitali ili takwimu kamili ipatikane na wale wajawazito watapatiwa zawadi kwa ajili ya kuwasaidia kujifungua salama.

Alisema ili kuandaa zawadi hizo ni lazima wapate idadi ya wanawake hao kwa ajili ya maandalizi ya siku hiyo muhimu.

Aidha, aliwataka wananchi wa Korogwe kuacha mtindo wa kutupa watoto na badala yake wajitahidi kutimiza wajibu wao wa kuwalea.

Alisema hivi karibuni wameokota kitoto kichanga na kufanikiwa kuokoa maisha yake na kwa sasa anaendelea vizuri baada ya kupatiwa huduma katika kituo cha afya.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Korogwe, Salma Swedi, alisema wanamshukuru Rais Samia amewafanyia mambo makubwa hasa katika sekta ya afya wamepokea Sh. bilioni 1.6 ambazo zimeelekezwa katika miundombinu mbalimbali ikiwamo jengo la dharura. Alisema jengo hilo limegharimu Sh. milioni 300 na limesaidia kuokoa dharura ambazo zinatokea barabarani ikiwamo ajali.

"Ujio wa jengo hilo umesaidia kupunguza adha kubwa kwa wagonjwa na kuokoa maisha yao. Pia tumeongezewa vituo vya afya viwili awali tulikuwa na kituo kimoja hivi sasa tuna vituo vitatu katika halmashauri hii," alisema.

# Serikali yasema imedhamiria kulinda uhuru wa habari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Idara ya Habari (Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, amesema serikali imedhamiria kulinda uhuru wa vyombo vya habari na kuhakikisha wanahabari wanatekeleza majukumu yao bila bughudha.

Msigwa alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akifungua mkutano wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika (MISA) pamoja na maadhimisho ya miaka 30 ya taasisi hiyo nchini Tanzania.

"Kwa kuthibitisha hilo kwa muda wa miaka miwili tangu aingie madarakani Rais Samia Suluhu Hassan, hakuna chombo chochote cha habari nchini ambacho kimefungiwa. Hii inaonyesha kuwa serikali imedhamiria kulinda uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza," alisema Msigwa.

Aidha, alisema serikali inataka kuifanya sekta ya habari nchini kufanya kazi zake bila vikwazo kwa kuzingatia sheria taratibu na kanuni za nchi.

"Ili kufanikisha lengo hilo hivi sasa serikali inaendelea na mchakato wa kuifanyia mapitio ya sheria na sera ya habari ili kufanyiwa marekebisho kulingana na mahitaji ya sasa" alisisitiza.

Msigwa alivitaka vyombo vya habari na wanahabari nchini kuzingatia sheria, kanuni na miongozi ya nchi ili kutekeleza majukumu yao ya kila siku bila kusumbuliwa.

"Pia suala maadili kwa waandishi wa habari linapaswa kuzingatiwa sana. Miaka 30 ya MISA Tanzania ni safari ndefu yenye mengi ya kujifunza. Tanzania imeshiriki katika safari hiyo yenye mafanikio na serikali inaendelea kuweka mazingira rafiki kwenye sekta ya habari pamoja na kuimarisha teknolojia ili kutoa mchango kwenye maendeleo," alisema.

Msigwa alisema hivi sasa kuna haja ya mafunzo kwa waandishi wa habari kuliko wakati wowote kwa kuwa tatizo la mlipuko wa vyombo vya habari vya mtandaoni limekuwa kikwazo, hivyo MISA na wadau wengine watie mkazo kwenye mafunzo ya wanahabari nchini.

Mwenyekiti wa MISA Tanzania, Salome Kitomari, aliipongeza serikali kwa kuchukua hatua mbalimbali za kuondoa vikwazo kwa waandishi wa habari.

"Serikali imeendelea kuhudumia taasisi za wanahabari bila ubaguzi hali inayowafanya waandishi kujisikia kuthaminiwa na kupendwa, na tunatoa pongezi kwa bajeti ya wizara kupitishwa," alisema.

Alisema azimio la kuanzishwa kwa MISA, lilitolewa Mei 3, 1993 Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari kwa jukumu kubwa la uhuru wa vyombo vya habari na ukusanyaji wa taarifa.

"Moja ya changamoto za wanahabari nchini ni uchumi wao kutokuwa mzuri. Waandishi wengi wana hali ngumu kimaisha, hawana mikataba, hawana bima, hawana stahiki zingine za mfanyakazi hali inayochangia baadhi yao kuangukia kwenye rushwa," alisema Kitomari.

## MSUGUANO NA MWL. NYERERE


# Dk. Slaa: Msimamo wangu ni ule ule, wananchi wasipangiwe idadi ya watoto

**Na Waandishi Wetu**

NI nadra kusikia jambo hili likizungumzwa na wanasiasa na hata viongozi wa serikali, lakini ni kweli kwamba miaka 1980, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere alipendekeza kuwe na Sera ya Watu.

Katika sera hiyo, Mwalimu Nyerere alitaka kuwekwe masharti kwamba kila familia isiwe na zaidi ya watoto wanne. Sera hiyo ilipingwa vikali na viongozi wa dini, akiwamo Dk. Wilbroad Slaa, aliyekuwa Katibu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC).

Kwenye ukurasa wa 57 wa kitabu kinachozungumzia maisha yake, alichokipa jina la 'NYUMA YA PAZIA', Dk. Slaa anaeleza namna alivyoingia katika msuguano na Mwalimu Nyerere wakati wa utumishi wake wa kanisa. Hiyo ni baada ya kumpinga Baba wa Taifa, kuhusu Sera hiyo ya Watu



Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere



Dk. Willibrod Slaa

Dk. Slaa anaweka wazi kuwa mazungumzo yake na Mwalimu Nyerere kipindi hicho yalikuwa yanafanyika majira ya saa 6-7 usiku na anaamini 'hakushughulikiwa' kwa kupinga sera hiyo kwa kuwa hata viongozi wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) waliipinga.

Hata hivyo, Dk. Slaa anaeleza kuwa msimamo wake huo ulifanya Mwalimu Nyerere atume ndege maalum kumfuata Musoma kwenda Dodoma Januari 6, 1989, kujieleza mbele ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwanini TEC ilipinga sera hiyo.

Wiki hii, baada ya miaka 34 kupita, Nipashe katika mazungumzo maalum na Dk. Slaa inahoji kama mwanasiasa huyo amebadili msimamo wake na kuunga mkono sera hiyo ya Mwalimu Nyerere.

Dk. Slaa ana majibu katika hilo, akieleza: "...hoja yangu ya msingi ni kwamba udhibiti wa ongezeko la watu ni uamuzi kati ya mwanamume na mwanamke. Si uamuzi wa serikali. Kumbuka wakati tunajadili hilo, China walikuja na sera kwamba akizaliwa mtoto wa kike anauawa.

"Kwanza (sera) ilikuwa mtoto mmoja kwa familia. Na akizaliwa wa kike anauawa kwa sababu anakwenda kutuzalia watoto wengine. Je, hiyo ni haki? Kwa hiyo Mwalimu wakati ule alikuja na sera za Urusi na China za ujamaa.

Kumbuka wakati huo mwalimu alikuwa amevutiwa na ujamaa, hivyo akaja na sera ya watoto wanne tu. Sasa mtanzania unamwambia watoto wanne. 'Mungu amenipa utajiri wa ng'ombe 1,000 halafu unasema watoto mwisho wanne tu!'

Mungu amekupa utajiri ule wa ng'ombe na watoto kwa sababu una uwezo wa kuwatunza. Ni tofauti na mtu mwingine katika kijiji kile pale - hana shamba, ikizidi sana ana robo ekari, yeye huyo sasa anapaswa kutumia busara yake aliyopewa na Mungu kwamba 'nitawalishaje nitakapokuwa na watoto zaidi?'

"Kwa bahati mbaya wa Afrika tulikuwa na imani kuwa kila mtoto anakuja na neema yake, jambo ambalo si kweli, ndiyo maana wengine wanakosa nguo lakini huo ni mpango wa baba na mama namna gani wapate mtoto wao."

***SWALI: Sasa tunashuhudia ongezeko kubwa la watu nchini. Tufanye nini kulikabili kama hatuitaki hii sera ya Mwalimu?***

**DK. SLAA:** Elimu tu itolewe kwa wingi. Yeyote ambaye amesoma masuala ya population growth (ongezeko la idadi ya watu) yanasema hivi - ukimpeleka binti darasa la kwanza mpaka la saba, anapunguza idadi ya watoto wa kuzaa. Yeye mwenyewe tu hata kama mwanamume anataka.

Atakudanganya atakwenda kupiga zile sindano, hakuambii. Nina uhakika humu wengine mnapiga hizo sindano (waandishi wanawake). Je, huwa mnawaambia waume zenu?

Hizo zipo. Wanajua lakini hawatungiwi sheria. Serikali ikishaingia katika mambo hayo ni serikali ya kidikteta. Mambo ya uzazi mwachie mtu mwenyewe. Mungu ametupa akili, busara na hekima ili tujiongoze kama binadamu.

***SWALI: Utawala wa Hayati Dk. John Magufuli ambao wewe ulikuwa balozi wake, unanyooshewa kidole kwa kubana demokrasia. Kwanini umekuwa kimya katika hili?***

**DK. SLAA:** Wakati huo Dk. Slaa alikuwa nani? Je, majukumu ya balozi ni nini? Ungeniambia labda 'Dk. Slaa ulipokuwa Sweden', hukutekeleza majukumu yako ya kibalozi.

Wakati huo mimi sihusiki na siasa ila unaweza kuniuliza niliwezaje kuimarisha uhusiano wa Tanzania na nchi nilizokuwa ninaziwakilisha na picha unaziona hapo ukutani. Jinsi nilivyoleta wafanyabiashara, kwa sababu ndiyo ilikuwa kazi yangu lakini sio siasa.

Hoja za kwenye mitandao huwa hazinisumbui. Mimi huwa ninasema Magufuli ni binadamu. Tutambue ana mabaya yake na mema yake. Kuna vitu vizuri alivyofanya. Kwa mfano, hebu nionyeshe hata mtu mmoja aliyewahi kufanya utafiti kuwa Magufuli hiki aliiba. Yupo?

Ni maneno na hisia. Sasa, kwa mtu kama mimi, ambaye nimeshughulika na masuala ya ufisadi ambao unakwenda mpaka katika kabati ya serikali unanyofolewa karatasi kule ndani, unaonyeshwa kuwa huu ni wizi! Mimi kelele za mtaani hazinisumbui.

Tatizo kubwa sana la Magufuli ambalo mimi ninaliona, ni kuminya demokrasia. Kumbuka mwaka 2015 mimi nilisimama jukwaani kama mnakumbuka, kabla sijaondoka.

Niliondoka Septemba Mosi, lakini baadaye nilirudi kwa sababu kulikuwa na kitengo cha CCBRT tulikuwa tunakifungua na JK (Rais Jakaya Kikwete). Kwa hiyo, nikarudi Oktoba, nilikuwa katika kipindi kimoja cha chombo cha habari, nikaulizwa nitoe tathmini na nilisema kauli moja kwamba kama ingekuwa uchaguzi ni kitu ambacho kina gia ya reverse kama gari, lakini uchaguzi sio hivyo, hatua moja ikishapita imepita.

Sasa nikasema katika hatua hiyo kwa kuwa hatuwezi kurudi nyuma, nikasema mimi hapa sioni anayefaa katika wote waliokuwa wanagombea.

Ingekuwa inawezekana tufute tuanze upya, lakini kwa kuwa hapakuwa na uwezekano kwa sasa tulionao kati ya Lowassa na Magufuli, maana ndiyo walikuwa wagombea wakubwa, mimi ninaona mwenye dhambi kidogo ni Magufuli na niliyasema makosa yake ikiwamo kutoa nyumba ya serikali kwa watu wasiostahili.

Katika suala la mikutano ya hadhara, Magufuli alidanganywa na mawaziri wake waliomweleza kuwa uchaguzi huko Marekani ukiisha, siasa zinaendelea bungeni na nilikwenda nikawahoji hao mawaziri wakaniambia 'sasa balozi nani wa kumwambia tena Rais arekebishe kauli yake kwamba tulichomwambia hakikuwa sahihi?'

Wakaniambia cha kufanya ikifika Januari 2020, watabadilisha ile sheria lakini ilipofika hawakubadilisha. Magufuli aliibeba kwa sababu inamfaa kisiasa lakini waliomwandalia ni mawaziri wake ambao ni wanasheria na walikiri kwamba wao ndiyo waliompotosha Rais.

Suala lingine la kuhusu ndege ambalo watu wanasema amepiga, ukimuuliza mtu amepiga ngapi, hajui! Sisi enzi zetu tulikuwa tunafuatilia kwa kina. Tulimbana Mwandosya akiwa Waziri wa Mawasiliano, mimi na Hamad Rashid tukajifanya wapigania uhuru wa Congo, tukaandika email Marekani kiwandani kufuatilia bei ya ndege ya Rais wakati huo, ndani ya dakika mbili kampuni iliyowauzia ndege ikatupa jibu la bei halisi ya ndege hiyo.

Tukamwabia waziri umetudanganya. Leo kuna anayefanya hivyo? Tukafanya hivyo, kupata bei halisi ili kumkosoe waziri ambaye ndani ya Bunge anaonyesha bei yake na sisi tukiwa na bei halisi.

Ingekuwa kuna mtanzania amefuatilia kwa kiwango hicho, hapo ningeelewa na hayo makosa anayafanya hata Lissu leo na nilimwandikia meseji juzi kwa mliouliza kuwa tunawasiliana. Tunawasiliana.

***SWALI: Zipo taarifa kwamba hauko sawa na familia yako. Kuna ukweli upi katika hili daktari?***

**DK. SLAA:** Nina watoto wawili na mama wa kwanza ambaye hatujafunga ndoa, Rose Kamili, ambao leo ni watu wazima. Baadaye nikafunga ndoa kule Canada na Josephine lakini tulikuwa tumeshapata mtoto wetu tukiwa huku na huyo mama sasa ambaye tulifunga ndoa (Josephine) tuna watoto watatu na Rose (watoto) wawili.

Hao wa Josephine wote wako Canada kwa sababu wanasoma. Mimi nilipokwenda Sweden, sikuweza kuwahamisha kwa sababu mifumo ya elimu inatofautiana na unajua katika kazi ya ubalozi, leo upo hapa miaka miwili kesho miaka mitatu uko kwingine. Sasa Sweden, kwa mfano, lazima kwanza ujifunze lugha yao mwaka mzima.

**Imeandikwa na Enock Charles na Zanura Mollel.**

# HABARI KITAIFA




Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Mohammed (kulia) na Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa Puma Energy Afrika, Ben Hassan Ouattara (kushoto), wakishuhudia utiaji saini makubaliano ya ushirikiano kati ya Meneja Mkuu wa Puma Energy Tanzania, Fatma Abdallah na Mkurugenzi wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST), Dk. Mahmoud Abdulwahab Alawi, Zanzibar jana. Puma Energy Tanzania itawekeza Sh. milioni 352 kusaidia programu ya mafunzo ya wahitimu wa miaka mitatu yenye lengo la kuendeleza sayansi na teknolojia kisiwani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

## TLS yaingilia kati sakata la wakili aliyezua purukushani

**Na Kulwa Mzee**

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kimeingilia kati ili kuchunguza purukushani kati ya Wakili Baraka Mukama aliyekuwa akizuia wateja wake kukamatwa na polisi.

Purukushani hizo zinazochunguzwa zimetokea Mei 23, mwaka huu, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu baada ya wateja wa Wakili Mukama kuachiwa huru chini ya kifungu namba 225 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Kwa mujibu wa barua hiyo ya uteuzi iliyotolewa na kutiwa Saini na Rais wa TLS, Harold Sungusia, chama hicho kimeteua timu ya mawakili wanne kuchunguza sakata la wakili huyo.

"Wanachama wa sekta ya sheria na haki, naandika kuwafahamisha kwamba kwa bahati mbaya tukio lililotokea Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu lilihusisha mtu aliyejitambulisha kuwa wakili na ofisa wa polisi.

"Liliripotiwa kuwa kulikuwa na mvutano wa kimwili kati ya wakili na polisi ndani ya eneo la mahakama. Kutokana na uzito wa jambo hilo na kwa heshima ya taaluma, kwa ruhusa ya Baraza la Uongozi TLS, nateua timu ya mawakili wafanye uchunguzi wa haraka wa tukio hilo.

"Timu itahusisha mawakili wafuatao, Margreth Mwihava Mwenyekiti wa TLS Ilala, Hekima Mwasipu, mtaalamu wa sheria za jinai, Emmanuel Augustino aliyekuwa Mwenyekiti TLS Dar es Salaam na Anastazia Muro ambaye ni Meneja wa Maslahi ya Wanachama wa TLS," alisema Sungusia.

Alisema timu hiyo ilichaguliwa kwa kuzingatia ukweli kuwa wajumbe hao wana utaalamu wa kutosha, wana ujuzi na weledi na hawataegemea upande mmoja katika kuhakikisha usawa katika uchunguzi wa haki.

Sungusia alisema walioteuliwa ni wanachama waaminifu wa TLS, wazoefu katika kushughulikia mambo nyeti yanayohusiana na haki.

"Uchunguzi una lengo la kukusanya taarifa husika na kutoa ushauri kwa baraza ya nini cha kufanya au kuamua," alisema.

Alisema walioteuliwa watakuwa na majukumu ya kutambua taarifa za Wakili Baraka Jafari Mukama yakiwamo majina, maelezo ya shauri alilokuwa analisimamia, jina na cheo na maelezo ya polisi aliyehusika katika purukushani.

Sungusia alitaja jukumu la pili kuwa timu itapaswa kufanya mahojiano na wakili huyo na wakati itakaporuhusiwa watamuhoji polisi muhusika na mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Alisema kwa kuongezea watafanya mahojiano na mtu yoyote ambaye alihusika au kushuhudia tukio au anazo taarifa kuhusiana na tukio hilo.

"Jukumu la tatu watachunguza sababu ya tukio na purukushani hizo kati ya polisi na wakili. Pia watapaswa kuchunguza mazingira yaliyosababisha purukushani hizo pamoja na taarifa yoyote iliyochangia purukushani hiyo," alisema.

Jukumu la nne, alisema ni kulingana na watakachokipata, timu inatakiwa kuja na ushauri wa kina kwa Baraza la TLS wa njia zitakazoweza kuchukuliwa kumaliza tukio hilo, ushauri huo utakuwa na lengo la kushughukia utovu wa nidhamu unaoweza kutokea, ukiukaji wa maadili au masuala ya kimfumo ambayo yanaweza kuwa yamechangia tukio hilo.

"Nawaomba wanachama wote wa TLS na wadau kutoa ushirikiano kwa timu hiyo sambamba na kutoa taarifa zitakazowawezesha kutekeleza majukumu yao vizuri, kupata suluhisho la uwazi na kwa wakati ni jambo muhimu litakaloimarisha imani ya jamii kwa taaluma ya sheria.

"Naamini uwajibikaji wa hii timu katika kulinda viwango vya juu vya taaluma na uaminifu katika jamii ya wanasheria. Natarajia matokeo mazuri ya uchunguzi, Baraza la uongozi la TLS watajikita katika ripoti itakayotolewa na hii timu wakati wanachukua hatua kuhusiana na tukio hilo,"alisema Rais wa TLS katika taarifa yake," alisema.

Vurugu hizo ziliibuka baada ya Mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Romuli Mbuya kuwaachia huru washtakiwa watatu waliokuwa wakikabiliwa na mashtaka ya kughushi stika za dawa mbalimbali wakionyesha ni halisi wakati si kweli.

Hakimu Mbuya alifikia uamuzi huo wa kuwaachia chini ya kifungu cha sheria namba 225 baada ya upande wa utetezi kupinga maombi ya Jamhuri ya kuahirisha shauri hilo.

Uamuzi huo wa Mahakama uliwafanya watuhumiwa Khalid Somole na Betty Mwankikusye kukimbia wakikwepa kukamatwa tena.

Washtakiwa wengine ambao hawakukimbia ni Raphael Lyimo na Abdiel Mshana.

Hata hivyo imebainika kuwa namba anazodai kutumia wakili huyo 4696 zinasoma jina ambalo si lake kwani namba hizo zinasoma jina la Wakili Nyando L. Nashon.

## Ndugu wa aliyejirusha ghorofani wafunguka

**Na Maulid Mmbaga**

NDUGU wa marehemu Joel Misesemo, maarufu MC Joe aliyefariki dunia kwa kujirusha ghorofani, wamebainisha kuwa ndugu yao kabla ya kukutwa na umauti alipatwa na ugonjwa wa kupooza upande mmoja na hakuwa mtu wa kuwashirikisha wengine matatizo yake.

Joel alifariki juzi baada ya kujirusha kutoka ghorofa ya saba katika jengo la Derm lililoko Makumbusho, jijini Dar es Salaam. Kutokana na tukio hilo Jeshi la Polisi limesema linaendelea kufanya uchunguzi ili kubaini sababu ya kifo hicho.

**MKE WA JOEL AFUNGUKA MAZITO**

Mke wa marehemu Joel, aliyejitambulisha kwa jina moja la Liz, amebainisha kwamba awali alikuwa na mgogoro na mume wake baada ya kumkatalia kuoa mke wa pili, akidai kuwa alikuta ujumbe mfupi wa maandishi na picha asizozielewa kwenye simu ya mumewe jambo lililosababisha kuwa na mikwaruzano baina yao.

Alibainisha hayo jana huku akidai kuwa alipoona ujumbe na picha hizo kwenye simu ya mumewe alimuita na kumuuliza jambo lililozua ugomvi mkubwa uliosababisha simu yake kuvunjwa na baada ya hapo aliondoka na kurudi nyumbani kwao.

"Niliondoka nikaenda kukaa nyumbani kwetu baadaye kaka yake alinipigia simu akasema shemeji tunakuhitaji nyumbani, tukaenda hadi kwao tukakalishwa kikao wakauliza tunaomba mtuambie tatizo ni nini? Mimi sikuweza kusema, nilikuwa nawaonea wazazi wake huruma, kama mzazi akiambiwa kwamba mwanao anafanya jambo hili inauma.

"Alikuwa na madhaifu mengi, lakini tulivumiliana, wanawake tunapitia mambo mengi alikuwa ananijali, lakini kuna vitu alikuwa anavifanya ambavyo nilikuwa siridhiki navyo," alisema.

**BABA YAKE AKANUSHA UVUMI**

Baba mzazi wa marehemu, Maxon Misesemo Chizii, alisema alizungumza na mwanawe Jumapili na taarifa za msiba alizipata Jumanne saa 5.30 asubuhi kupitia kwa kaka yake marehemu kuwa mdogo wake amefariki dunia kwa kujirusha toka ghorofani.

Chizii aliyewahi kuwa Katibu wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma na pia Mkurugenzi wa Uchaguzi wa CCM, alisema kifo cha mwanawe kimemshtua sana.

"Nilishtuka sana kwa kweli, pale kwenye ghorofa ndipo mahali ambapo ofisi yake ilipo. Sikuwa na wasiwasi kwa kuwa alikuwa amekwenda kwenye ofisi yake. Nilipopata habari hiyo ilibidi niende nyumbani kwake Mwananyamala kufuatilia na wao walisema hawana taarifa zaidi, lakini polisi waliwahi na kuthibitisha kuwa amekufa kwa njia hiyo," alisema.

Aliwataka wananchi kuacha kusikiliza habari za uzushi, kwa sababu mwanawe alikuwa mpenzi wa familia, anasaidiana na watu na kifo chake kimeonekana kwenye kamera za CCTV hatua kwa hatua.

**MTOTO ALIYELELEWA NA JOEL**

Akizungumza na waandishi wa habari jana, binti aliyelelewa na Joel, Janeth Andendekizi alisema, siku moja kabla ya kifo cha Joel aliwasiliana naye na aliposikia sauti yake alihisi kuwa hayuko sawa, alipomuuliza kama anaumwa alimjibu hapana.

"Siku za nyuma nikiongea naye alikuwa ni mtu mchangamfu, lakini nilipozungumza naye mara ya mwisho sauti yake haikuwa sawa nilipomuuliza mbona sauti yako iko hivyo? Unaumwa?

Alisema hapana yuko sawa japo hajisikii vizuri," alisema; "Pia nilimuuliza uko wapi? Akasema yuko Makumbusho. Nikauliza umeweza kutoka maana Jumapili aliniambia kuwa hajisikii vizuri, akasema ameweza kutoka na ameendesha gari, ikabidi nimpigie bibi ambaye ni mkewe maana nilikuwa na wasiwasi amewezaje kuendesha gari wakati alisema anajisikia vibaya," alisema Janeth.

Baada ya kuwasiliana na mkewe alimtaarifu kwamba Joel alikuwa anaumwa mwezi mzima uliopita.

Janeth alisema, siku iliyofuata alipata taarifa kwamba Joel amefariki. "Ilinibidi nije nyumbani haraka nilipofika niliambiwa kwamba baba asubuhi aliamka hakumuaga mtu akaondoka tu hawakujua ameenda wapi, mama akajaribu kumpigia simu hakupatikana.

Naye Samuel Sasali, ambaye alikuwa mtu wa karibu na Joel, alisema moja ya vitu vilivyomuweka karibu sana na marehemu ni namna ambavyo alikuwa akijishughulisha na kujitoa katika kuwasaidia watu wengine.

"Kwanza kila mtu haamini kitu kilichotokea, hatujajua kweli ni yeye mwenyewe aliamua kufanya hivyo, amesukumwa au ni nini, alikuwa mchangamfu, yani hata leo nikikutambulisha kwakwe atakuchangamkia kama mlifahamiana muda mrefu," alisema Sasali.

"Lakini Joel alikuwa sio mtu wa kupenda sana kushirikisha wengine shida zake, yani ni mtu ambaye alikuwa anaamini kwamba anaweza kupambana nazo, mara ya mwisho nilikutana naye, lakini hatukuongea kwamba ana matatizo, kwa hiyo inawezekana katika hili jambo labda alikuwa na stress, changamoto au kuna mambo yalikuwa yamemtinga," alisema Sasali.

"Kilichoniuma niliposikia stori kwamba Joel amejiua kwa kujirusha yani niliona hiyo ni adhabu kali sana, kwasababu alikuwa ni mtu wa watu, kwenye haya maisha kila mtu anachangamoto zake."

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari ichukuliwe dhidi ya majanga katika majengo

**WIKI** hii mkoani Dar es Salaam, kuna matukio mawili yaliyofuatana ndani ya siku mbili na maeneo yaliyo karibu. Matukio hayo ni mwananchi mmoja kujirusha kutoka ghorofa ya saba katika jengo la Derm Plaza, Kijitonyama na kupoteza maisha na lingine ni watu saba kujeruhiwa katika jengo la Millennium Tower, Makumbusho. Majengo hayo yanatazamana na yako kando ya barabara ya Ali Hassan Mwinyi.

Haijafahamika sababu za kijana huyo ambaye pamoja na mambo mengine alikuwa mshereheshaji (MC) kujitoa uhai. Lakini sababu ya watu waliojeruhiwa kwenye lifti ni kwamba chombo hicho ambacho hupandisha na kushusha watu kilikosa breki. Sambamba na kukosa breki, ilielezwa kuwa lifti hiyo ilikuwa katika matengenezo na kwamba haikujaribiwa kama imeimarika kabla ya kuruhusu watu kuipanda.

Kwa mujibu wa wataalamu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, lifti hiyo haikutakiwa kubeba watu kabla ya kujihakikishia kuwa ina uwezo na badala yake wasimamizi walipaswa kuijaribisha kwa kushusha na kupandisha mizigo, jambo ambalo halikufanyika.

Tukio la watu kujeruhiwa au kunasa kwenye lifti si la kwanza kutokea nchini bali ni la muda mrefu. Ziko taarifa zilizotolewa kuhusu lifti katika majengo mbalimbali kukumbwa na hitilafu, hivyo kusababisha watu kupata matatizo mbalimbali ikiwamo kukosa hewa na kujeruhiwa kama ilivyotokea juzi.

Mbali na lifti katika majengo, tatizo lingine ambalo limekuwa la muda ni vyombo vya moto hasa vya majini kwa maana ya vivuko kukumbwa na changamoto ya kuzimika na wakati mwingine abiria kukumbwa na taharuki wakiwa katika vyombo hivyo. Iko mifano mingi ya vivuko hivyo katika Bahari ya Hindi na maziwa kama Victoria na Tanganyika vyombo hivyo kupata hitilafu katikati ya safari. Sababu za kutokea hitilafu hizo zikiwamo kuzimika kwa injini vikiwa na abiria ni kutokuwapo kwa ukaguzi, huduma (service) na matengenezo ya mara kwa mara ndiyo maana majanga kama hayo hutokea.


Hivi sasa kuna ongezeko la majengo ya ghorofa katika miji mikubwa, Dar es Salaam ikiwamo, hivyo ni vyema miundombinu kama lifti na umeme ikasimamiwa ipasavyo wakati wa ujenzi wake. Hatua hiyo itasaidia kwa kiasi kikubwa kupungua majanga yanayoweza kutokea na kusababisha maisha ya watu kupotea. Ni vyema mamlaka na taasisi zinazosimamia ujenzi na masuala ya ufundi zikawajibika ipasavyo ili kuhakikisha majanga yasiyo ya lazima yanaepukika.

Katika kuhakikisha hayo yanafanyika, kila hatua ya ujenzi na ukaguzi ufanyike kwa lengo la kujiridhisha kuwa masuala ya viwango yanafuatwa. Baada ya kukamilika, taasisi kama zimamoto na uokoaji, zifanye ukaguzi wa mara kwa mara ili kuona kama suala la usalama linazingatiwa kwa maana ya kuwa na vifaa vya kuzimia, mfumo imara wa umeme na kama majengo ni marefu lifti zinafanya kazi na zinafanyiwa ukarabati na matengenezo mara kwa mara.

Aidha, katika vyombo vya majini, Wakala wa Umeme na Ufundi (TEMESA) ihakikishe vinakaguliwa mara kwa mara pamoja na kufanyikwa matengenezo. Ni Imani kwamba kwa kufanya hivyo, majanga mengi yanaweza kuepukika na kuwafanya wananchi na watumiaji wengine kuwa salama.

Wahenga wanasema ni heri kuzuia kuliko kutibu, hivyo kuwapo kwa ukaguzi na matengenezo ya mara kwa mara ya vyombo vya usafiri na lifti katika majengo, kutazuia kwa kiasi kikubwa majanga kama lile lililotokea juzi na kuzua taharuki miongoni mwa wananchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Serikali na wataalamu saikolojia, wavalie njuga kasi ya watu kujiua

Na Adam Fungamwango

**KILA** ukiamka, ukianza kusikiliza vyombo vya habari na kusoma magazeti, moja ambalo utakutana nalo kwa miaka ya hivi karibuni nchini ni watu kujiua au kuua wenzao.

Limeanza kuonekana si jambo la ajabu tena kwani angalau moja ya habari kama siyo mbili tatu, utakuta mtu kamuua mwenzake kwa sababu mbalimbali, pesa au mapenzi, au mwingine kujiua mwenyewe kwa sababu kama hizo, au zinazofanana. Hata wale ambao baadhi yao wanafanya hivyo, wanawafanyia watu ambao ni wa karibu yao kabisa. Baba anaua mwanaye kwa sababu kaiba shilingi 500 tu, mama kamuua binti yake kwa sababu kadokoa mboga, utasikia mtu kamuua mkwe, mumewe, rafiki yake nakadhalika.

Upande wa pili, ndiyo utasikia mtu amejiua mwenyewe, lakini kabla ya hapo kamuua mkewe kwanza na watoto. Wengine ndiyo wanajimaliza kwa kunywa dawa za wadudu, za binadamu kwa dozi kubwa, sumu na wapo wanaokwenda kujirusha maghorofani.

Kuanza kulizoea na kutoshangaza watu sana, badala yake kuwa stori tu za kawaida si jambo jema kwa nchi yetu, kwani miaka ya huko nyuma habari kama hizi watu walizisoma kwenye nchi za wenzetu na si hapa. Na kama litatokea nchini basi linaweza kuwa tukio ambalo litazungumzia kwa mwaka mmoja au zaidi na litaonekana kama vile ilikuwa jana. Mfano maeneo ya Manzese, Dar es Salaam miaka ya mwanzoni mwa 1980, kulitokea vurumai kiasi cha kuuawa mtu, lakini kwa sababu ni ghalabu sana matukio hayo kutokea, ilibaki simulizi na lile eneo hadi leo linaitwa Manzese Soweto, wakifananisha na mauaji yaliyotokea kitongoji cha Johannesburg nchini Afrika Kusini, Juni 16, 1976 zaidi wa wanafunzi 170 waliuawa na askari wa utawala wa Makaburu wakati huo.

Hii inaonyesha kuwa zamani matukio kama haya yalikuwa ni nadra sana na yakitokea inakuwa si rahisi kufutika kwenye mioyo ya wananchi au wakazi husika wa maeneo hayo.

Kwa sasa yamekuwa mengi kiasi cha kuonekana ya kawaida na kusahaulika. Kwa sababu leo linatokea hili wakati watu wanajadili kesho kutwa lingine.

Mauaji na kujiua si jambo la kuliachia Jeshi la Polisi peke yake, kwa sababu lina mambo mengi sana ndani yake. Wakiachiwa polisi sana sana watakuwa tu wakiokota maiti, na kukamata watuhumiwa kabla ya kuwapeleka mahakamani. Tatizo bado litakuwa halijatatulika. Ni suala sasa la madaktari na wataalam wa masuala ya saikolojia, wakishirikiana na serikali kukaa na kuangalia tatizo hasa linaloikumba jamii ni nini?

Na kwanini zamani hakukuwapo mambo kama haya? Tusije na dhana dhaifu kuwa miaka ya nyuma hakukuwa na vyombo vingi vya habari hivyo yalikuwa hayaripotiwi, tuje na majibu ya kisayansi.

Inaonekana kama kuna kitu hakipo sawa kwa vijana na watu wa rika ya kati.

Kujirusha kutoka ghorofani hivi karibuni kwa mtu mmoja maeneo ya Makumbusho Jijini Dar es Salaam, kumezua upya wasiwasi, kuwa watu wanakuwa na mambo mengi kichwani ambayo hawana pa kuyapeleka.

Haingii akilini mtu mwenye akili yake timamu afanye jambo lile la hatari kama hana msongo wa mawazo ambao inawezekana hajawahi kumwambia mtu yeyote yule, na ingeweza kuwa ni tiba sana kwake. Mtu mmoja alikimbiwa na mkewe, akataka kujinyonga, lakini kabla ya kufanya hivyo akamwambia rafiki yake. Rafiki yake akampeleka kwa ndugu yake ambaye alikimbiwa na mkewe aliyebeba vitu vyote ndani pamoja na watoto.

Jamaa analala chini, lakini akamwambia siku si nyingi atanunua kitanda na maisha yataendelea. Aliyetaka kujinyonga akaahirisha kwa kuona afadhali yeye amekimbiwa lakini kila kitu ndani kipo kuliko huyu mwenzake.

Nashauri kwenye hospitali zote na maeneo mbalimbali kama ustawi wa jamii, serikali kwa kushirikiana na madaktari ianzishe vitengo kama vile vya majukwaa ya kijinsia, ili kukaribisha watu wenye msongo wa mawazo kwa ajili ya ushauri nasaha, faraja na maelekezo mengine ya kitaalam ili kulinda na kuokoa maisha ya watu wenye matatizo kama hayo ambayo hawana mahali pa kuyapeleka, labda kwa kuona yanaweza kusambazwa kwa watu wasiohusika.

Hii itaokoa maisha ya wananchi ambao wengi wao si wasomi tu na wanaotegemewa na familia zao, lakini ni nguvu kazi ya taifa na inahitajiwa nchini kwenye ujenzi wa maendeleo ili kazi iendelee.




Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii Tiba Taifa, Abdulmalik Mollel, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Global Education Link na Global Medicare (katikati), akiongoza ujumbe wa madaktari bingwa kutembelea moja ya hospitali za nchini India jana walipokwenda kwa ajili ya kuangalia fursa za kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii.
**PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Akana kisu anachodaiwa kumuulia mpenziwe

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA Ally Balanda, maarufu kwa jina la Idofolo, ameieleza mahakama kuwa kisu ambacho anadaiwa kumuulia mpenzi wake, aliyekuwa Mwalimu wa Shule ya Msingi iliyoko Tabata, Selan Kondo, hakina alama yeyote inayoonyesha umiliki wake.

Aidha, kwenye maelezo ya onyo, mshtakiwa huyo anadaiwa kuwa alikiri kutembea na kisu hicho siku tatu akimwinda Selan ili amchome nacho na kwa maandalizi hayo alikuwa amekinoa.

Balanda alidai hayo juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Franco Kiswaga, wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakati akitoa utetezi wake katika kesi ya mauji ya Selan Kondo, baada ya mashahidi wanane wa upande wa mashtaka kumaliza kutoa ushahidi wao.

Akiongozwa na wakili wake, Roman Lamwai, Balanda alidai kuwa kisu ambacho kilizungumziwa na shahidi wa upande wa mashitaka na kutolewa kama kielelezo mahakamani hapo, hakina alama inayoonesha umiliki wake.

"Kisu hiki hakina tofauti na visu vingine vinavyokuwapo sokoni kwa mara ya kwanza. kisu hiki nimekiona hapa mahakamani. Na kuhusu hii leso ambayo inadaiwa kuwa ni ya kwangu haina alama inayoonesha umiliki wangu," alidai Balanda.

Pia alidai kuwa hafahamu vitu hivyo vilifikiaje eneo la tukio na pia hajawahi kufanyiwa gwaride la utambuzi. Kuhusu Haruna Mmari ambaye alidai kuwa alimtambua yeye, hakuwahi kuonekana mahakamani kuthibitisha hilo.

Mshtakiwa alidai kuwa hajawahi kuandika maelezo ya onyo na kwamba kwa sababu walimpiga sana, walimlazimisha kutia saini maelezo hayo ndiyo maana Saini za dole gumba zinatofautiana.

Kuhusu kufikishwa kwa mlinzi wa amani, alidai kuwa ni kweli alifikishwa Mahakama ya Mwanzo Buguruni ba baada ya hakimu kumwona ana uvimbe juu ya jicho, alisema ataishia hapo alipoishia, kwa hiyo nyaraka za mahakama hiyo hazitambui kuanzia ukurasa wa nne hadi 29.

"Kwa kuwa hakuna mtu yeyote aliyethibitisha kuwa mimi nina hatia, naomba mahakama iniachie huru," aliomba Balanda.

Akijibu maswali ya upande wa mashitaka, Balanda alidai kuwa hafamu kama katika kumbukumbu za Kituo cha Polisi alichowekwa mahabusu baada ya kukamatwa, kinaonyesha kuwa alikamatwa Mei 10, 2019 kwa sababu anajua alikamatwa Mei 8,2019.

Kadhalika, alidai kuwa wakati alipopigwa na polisi hakuzimia bali alipata maumivu na kwamba alikamatwa Kimara nyumbani kwa ndugu yake, alikokwenda kusalimia na hadi anakamatwa alikuwa anaishi Tabata Mwananchi.

Hata hivyo, alidai kutengana kwao hakukusababishwa na kutoelewana baina yao na hakuwahi kumbembeleza warudiane kwa sababu hakuridhika na kuachana kwao kutokana na kwamba tayari mwanamke huyo alishamfanyia mambo mengi.

Baada ya mshitakiwa kumaliza kujitegemea, wakili wake, Lamwai, alidai kuwa hawana shahidi mwingine na pia pande zote mbili zimeieleza mahakama kuwa hazitakuwa na majumuisho ya mwisho, kwa hiyo mahakama ikapanga kutoa hukumu Juni 28, mwaka huu.

Balanda anayetuhumiwa Mei 6,2019 akiwa eneo la Tabata Liwiti ndani ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, alimuua Selan Kondo.

# Lugha alama kuingizwa kwenye mitaala

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI ina mpango wa kuingiza lugha ya alama kwenye mitaala ya elimu nchini ili kutatua tatizo la mawasiliano kwa wanafunzi wasiosikia.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Stella Ikupa kwa niaba ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Ikupa alihoji mpango wa serikali kuingiza lugha ya alama kwenye mitaala ya elimu nchini.

Naibu Waziri alisema katika mchakato wa mapitio ya sera na mitaala unaoendelea somo la lugha ya alama limependekezwa liwe la lazima kwa walimu wote tarajali katika vyuo vyote vya ualimu na vyuo vikuu nchini.

"Pamoja na kuwapo kwa mpango na mapendekezo hayo, tayari serikali imeandaa na kusambaza kamusi ya lugha ya alama ya Tanzania ya kidijitali katika shule na vyuo vinavyopokea wanafunzi viziwi," alisema.

Aidha, alisema kozi ya lugha ya alama ya Tanzania inatolewa katika Chuo cha Ualimu Patandi na Kabanga na katika vyuo vikuu vya Dodoma, Dar es Salaam na Archbishop Mihayo University College Tabora (AMUCTA) kwa lengo la kumudu darasa jumuishi.

"Serikali imeendelea kutoa mafunzo kwa walimu wa elimu maalum na wasio wa elimu maalum 3,650 wa shule za msingi na sekondari kwa lengo la kuwajengea uwezo wa namna bora ya kuwafundisha na kuwahudumia wanafunzi viziwi ili kujenga jamii jumuishi ya viziwi shuleni," alisema.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**






Rais wa Wentworth Africa Foundation, Barbara McBean akifurahia na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mwanagati, wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam, baada ya taasisi hiyo kuwakabidhi taulo za kike (pedi) wasichana 530 shuleni hapo hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Waziri serikali ya Nyerere afariki dunia

**Na Sabato Kasika**

ALIYEWAHI kuwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo katika serikali ya awamu ya kwanza chini ya Mwalimu Julius Nyerere, Herman Kirigini (pichani), amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Akiwa njiani kwenda msibani juzi, mmoja wa watoto wa marehemu, Rosemary Kirigini, aliiambia Nipashe jana kuwa baba yake alifariki juzi jioni mjini Musoma wakati akipelekwa hospitalini.

"Baba ameugua tangu mwaka 2014, akisumbuliwa na kisukari kilichosababishwa macho kupofuka, lakini pia baadaye akapata magonjwa mengine ambayo hayakujulikana," alisema Rosemary.

Rosemary alisema baba yao ambaye pia aliwahi kuwa Mbunge wa Musoma Vijijini mwaka 1980 hadi 1985, aliyezaliwa mwaka 1945, ameacha watoto tisa, wa kike wakiwa watatu na wa kiume sita.

Kwa mujibu wa Rosemary, maziko ya Mzee Kirigini yanatarajiwa kufanyika kesho Jumamosi kijijini kwao, Muryaza wilaya Butiama.

**MKONO KUZIKWA JUMATATU**

Aidha, mwili wa mbunge wa zamani wa Butiama mkoani humo, Nimrod Mkono, unatarajiwa kuzikwa Jumatatu ijayo, kijijini kwao Kigori Busegwe wilayani Butiama.

Mwili wa wakili na mwanasiasa huyo huyo, unatarajiwa kurejeshwa nchini keshokutwa kutoka Marekani. Ibada ya kuaga mwili itafanyika nyumbani kwake, Masaki, Dar es Salaam, kisha kuagwa Jumapili katika ukumbi wa Karimjee.

Ratiba hiyo imetolewa na Stephen Wasira, Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Kuratibu Mazishi ya mwanasiasa huyo aliyefariki dunia Aprili 18, mwaka huu, nchini Marekani alikokuwa akipatiwa matibabu.



"Hiyo ndiYo ratiba nilio nayo kwa sasa. Kama kutakuwa na mabadiliko nitawajulisha, lakini baada ya kuagwa pale Karimjee mwili utasafirishwa kwenda kuzikwa Butiama Jumatatu," alisema Wasira.

# Mawaziri wakutana na wazalishaji wa mafuta ya kula

**Na Joseph Mwendapole**

MAWAZIRI watatu wamekutana na wafanyabiashara jijini Dar es Salaam na kuweka mikakati ya kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kupikia nchini.

Mawaziri hao ni Waziri wa Uwekezaji, Viwanda, Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, Waziri wa Kilimo, Husssein Bashe na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba.

Akifungua kikao hicho juzi, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Kijaji, alisema lengo la kikao hicho ni kupata mawazo ya wafanyabiashara hao kuhusu namna ya kuboresha uzalishaji wa mafuta nchini.

Alisema serikali inataka kuona wafanyabiashara nchini wanazalisha mafuta yanayojitosheleza na kuacha kutumia fedha za kigeni kuagiza nje ya nchi.

Alisema kwa sasa alizeti imeshuka thamani kwa asilimia 50 na mafuta ya kupikia kwa asilimia 17 jambo ambalo limesababisha wananchi hususani wakulima kuwa na malalamiko. Dk. Kijaji alisema malalamiko ya wananchi yameisukuma serikali kukutana na wafanyabiashara hao ili kupata suluhisho.

"Tuna viwanda 771 vinavyochakata mafuta, tunazalisha tani 300,000 na mahitaji yetu ni tani 560,000 kwa hiyo mafuta bado hayatoshi hali inayotulazimu turuhusu wengine waagize ya kutoka nje ya nchi," alisema.

Dk. Kijaji alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alielekeza kuwe na mikoa mitatu ya kilimo cha alizeti ambayo ni Dodoma, Singida na Simiyu, lengo ikiwa ni kutafuta malighafi ya kutosha kuzalisha mafuta.

Pia alisema nguvu imewekwa kwa wakulima na wamefanikiwa kuzalisha alizeti ya kutosha na lengo ilikuwa kufikia uchumi shirikishi na kupitia kikao hicho wataondoa changamoto ili kukuza uchumi wa pamoja.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema ili kuondokana na changamoto hiyo kuna haja ya kuweka sera ya kuwakuza kiuchumi wafanyabiashara na hilo likifanyika ndani ya miaka mitatu serikali haitaagiza mafuta nje ya nchi.

Aliwataka wazalishaji wa mafuta ya alizeti kuwaripoti maofisa wa serikali wanao waomba rushwa ili waweze kuchukuliwa hatua.

"Natamani tufanye vizuri sisi wazalishaji tuondoke kwenye umimi bali wote tuangalie tunapata nini kwenye huu mnyonyoro wa samani na hivyo viwanda vilivyofungwa inasikitisha sana wengine ni vitisho vya hao maofisa wa serikali ambao mnashindwa kuwaripoti," alisema Dk. Mwigulu. Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema wazalishaji wa mafuta wanapaswa kukutana na kuchagua uongozi mzuri ambao utawasaidia kuwaunganisha na serikali wanapopata changamoto.

"Ninachotaka kuwaambia hapa mbele ya waziri ni kwamba wachakataji wa mafuta ya alizeti waanzishe taasisi ambayo itakuwa na umahiri wa kuwasilisha changamoto zao na kisiwe kama chama cha uanaharakati," alisema Waziri Bashe.

Baadhi ya washiriki wa kikao hicho walisema kuwa wanatarajia mapinduzi makubwa ili waweze kufanya uzalishaji ulio bora wa mafuta.

Nelson Mwakabuta, Meneja wa Kampuni ya Mount Meru, alisema wamefurahishwa na kikao hicho na wana uhakika changamoto zilizowakabili, ikiwamo upungufu wa malighafi na masoko yanaenda kupatiwa ufumbuzi.

"Tunaona taswira njema kupitia kikao hiki kwani tutapata mbegu ya uhakika, kiwanda kufanya kwa muda mrefu bila kutegemea msimu," alisema Nelson Mwakabuta.

Fatuma Salum, alisema kikao hicho kimeleta tija kwa wazalishaji wa mafuta kutokana na majibu na mikakati iliyotolewa na serikali.

Aliiomba serikali kuwapa ushirikiano wafanyabiashara kila wanapowasilisha changamoto zao hali itakayosaidia kuinua uchumi wa nchi.

# Tuzo kuwatambua vinara utunzaji mazingira yaja

**Na Jenifer Gilla**

ASASI za kiraia nchini kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, zimeandaa Tuzo ya Watu na Mazingira (WAMA), yenye lengo la kutambua juhudi za wadau katika kuhifadhi mazingira nchini.

Asasi hizo ni Tanzania Sustainable Development Initiative (TSDI), Environmental Consultancy (ELCA), Environmental Conservation Community of Tanzania (ECCT) na Taasisi ya Utu na Mazingira (HUDEFO).

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, mmoja wa waratibu wa tuzo hizo, Mkurugenzi wa TSDI, Fredy Kwezi, alisema hafla ya kukabidhi tuzo hizo zinatarajiwa kutolewa siku ya Mazingira Duniani ambayo huadhimishwa Juni 5, kila mwaka.

Aidha, alisema utoaji wa tuzo huo unatarajiwa kutolewa kila mwaka ili kuongeza chachu kwa wadau wa mazingira kuhifadhi rasilimali hiyo muhimu inayogusa kila sekta ya mwanadamu na kufikia malengo yaliyojiwekea serikali ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Tuzo hii ni ya kipekee yenye lengo kuu la kutambua na kuthamini juhudi za wadau mbalimbali, ikiwamo mchango wa mtu mmoja, kampuni, taasisi za umma na binafsi na taasisi za kiraia katika sekta ya mazingira ndani ya taifa letu," alisema Fredy.

Mkurugenzi wa ELCA, Caroline Manyama, alisema mchakato wa kukabidhi kwa washindi wa tuzo utatanguliwa na matukio kadhaa ya utunzaji wa mazingira, ikiwamo kufanya usafi katika fukwe na maeneo ya umma wenye kulenga kutoa elimu na ufumbuzi wa changamoto za kimazingira.

Alisema pia kutakuwa na maonyesho ya bidhaa na huduma rafiki kwa mazingira, mafunzo ya darasani na vitendo ya namna ya kuhifadhi mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na kongamano la mazingira litakalobeba ujumbe wa siku ya mazingira.

"Niseme tu tumeshaanza, Mei 28 na 29 tutakuwa na maonyesho ya bidhaa na huduma rafiki kwa mazingira katika viwanja vya posta eneo la sayansi chini ya udhamini wa Shirika la Mawasiliano la Taifa (TTCL). Wauzaji na watoa huduma wote rafiki kwa mazingira. Tunawakaribisha watu wote na hakuna gharama yoyote," alisema Caroline.

Mkurugenzi wa HUDEFO, Sarah Pima, alisema tuzo hizo zinatoa fursa kubwa kwa kampuni, taasisi na wafanyabiashara binafsi kujitangaza na kukutana moja kwa moja na wadau mbalimbali katika sekta ya mazingira na kuwakaribisha wadau wote wa mazingira kujiandikisha ili kutambulika michango yao katika utunzaji wa mazingira.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Muheza, kata ya Masuguru, wilayani Muheza mkoani Tanga, Benard Luanda (kushoto), akionyesha kwa waandishi wa habari majengo ya madarasa yaliyokarabatiwa na Mbunge wa Muheza ambae ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA' kwa gharama ya Sh. milioni 4.5, walipotembelea shuleni hapo mapema wiki hii. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Hifadhi ya Kilimanjaro kuingizwa orodha ya maeneo yenye upekee

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MCHAKATO wa kuingiza Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro (KINAPA) katika orodha ya maeneo ya kimataifa yenye upekee na yanayojumuisha uhifadhi na maendeleo endelevu ya jamii duniani 'umeiva.'

Tayari, Mtandao wa Global Geopark, unaofanya kazi, chini ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) limethibitisha.

Akizungumza jana katika Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, wakati wa kikao cha kukusanya maoni juu ya mchakato huo, Mhifadhi Mkuu wa Utalii wa KINAPA, Mweta Mweta, alisema hifadhi hiyo imeingizwa katika mchakato huo kwa kuwa ni miongoni mwa maeneo yenye utajiri mkubwa wa miamba ya aina mbalimbali.

"Kutokana na sifa hiyo, Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro, inakidhi vigezo vya kuwa miongoni mwa maeneo ya Mtandao wa Global Geopark, hadhi inayotambulika na Shirika la UNESCO.

Zaidi alifafanua, "TANAPA (Shirika la Hifadhi za Taifa) kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya UNESCO (NATCOM), limepanga kuingiza baadhi ya hifadhi za taifa za Tanzania ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro kwenye mtandao wa huo wa Global Geopark."

Kwa mujibu wa Mweta, miongoni mwa vigezo vya eneo kuingizwa kwenye mtandao huo wa kimataifa ni kufanya utambuzi wa vituo vya utalii vilivyomo ndani na nje ya hifadhi kwa ajili ya kuvitangaza.

Hatua hiyo, itaiwezesha hifadhi hiyo kuingia katika orodha ya dunia ya kijiolojia itakayotambuliwa na Umoja wa Mataifa, hivyo kuaminiwa kimataifa na kuwezesha kutembelewa na watu wengi wakiwemo watalii. Kutokana na vigezo hivyo, timu ya wataalam wa TANAPA na UNESCO-NATCOM, imeanza mchakato wa kuandaa andiko la kuomba UNESCO kuusajili Mlima wa Kilimanjaro kuwa katika mtandao wa Global Geopark.

# Serikali kupeleka timu ya kupambana na ukatili Manyara

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI imesema itatuma timu ya wanasheria, wasaidizi wa kisheria na mawakili wa serikali kukaa kwa siku 10 katika kila Halmashauri ya Mkoa wa Manyara, kupambana na vitendo vya ukatili.

Jana, Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria, Pauline Gekul, alisema uamuzi huo unalenga pamoja na mambo mengine kuzuia uvunjifu wa sheria na haki za binadamu,.

Gekul aliahidi hayo alipokwenda kuzungumza na wananchi Mjini Babati, wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Samia Legal Aid.

"Tumeanzisha hii kampeni inayoendeshwa na wizara ili kuongeza wigo wa kusikiliza kero za wananchi zinazohusu ukiukwaji wa haki na kuwasaidia bure.

"Watoto wanabakwa (kunajisiwa) na kulawitiwa. Katika kampeni hii, tutatoa ushauri na elimu ili watu waelewe na kesi zifunguliwe."

Awali, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Khatibu Kazungu, alisema kampeni hiyo ya Samia Legal Aid, itafanyika kwenye mikoa saba nchini. Kazungu, alisema kwenye kampeni hiyo watashirikiana na viongozi wa serikali, wasaidizi wa kisheria, viongozi wa dini na wananchi.

Vilevile, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Hadija Shaban, alisema kampeni hiyo itakuwa msaada mkubwa na itaokoa gharama kubwa, ambazo wananchi wanazitumia kufatilia haki zao na kesi.

Naye, Mwenyekiti wa kampeni hiyo kitaifa kutoka Shirika la Legal Service Facility (LSF), Aman Manyelezi, alisema ili kusaidia wananchi kupata msaada wa kisheria, wasaidizi wa kisheria 4,000 wamenolewa na mashauri zaidi ya 60,000 yalitatuliwa mwaka mzima.

# TPHPA yazuia uingizaji vipando visivyokuwa na ubora

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MAMLAKA ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA), imekataa ombi la kuingiza nchini vipando sita, kati ya 762 vilivyoombewa vibali vya kuingiza, huku ikieleza kuridhishwa na uchunguzi wa sampuli 103 za maabara na vitalu nyumba kukidhi viwango vya kimataif

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa (TPHPA), Prof. Joseph Ndunguru, katika mwaka wa fedha 2022/23 walikagua shehena za vipando 189 na kugundua zimekidhi viwango vya matakwa ya afya ya mimea na siyo kama ilivyodhaniwa, na hivyo kuruhusu biashara hiyo kufanyika.

Prof. Ndunguru, alikuwa akizungumza katika mahojiano maalumu na Nipashe kuhusu afya ya mimea na hatma ya sekta ya kilimo nchini.

"Kwa Tanzania, afya ya mimea ni muhimu sana kwa sababu tukiwa na udhibiti wa visumbufu mahiri, tutaongeza tija, ajira na pia kupunguza umasikini na kukuza uchumi wa nchi, kwa vile malighafi ya viwanda itaongezeka kwa sababu asilimia 60 ya malighafi inayoingia kwenye viwanda inatokana na sekta ya kilimo.

"TPHPA tulipokea jumla ya maombi 762 ya vibali vya kuingiza vipando nchini, ambapo kati ya hivyo vibali 756 vilitolewa sawa na asilimia 99.2

"Pia tulitoa mafunzo kwa wananchi 3,100 na maofisa ugani 900 katika udhibiti wa mdudu kanitangaze. Aidha, tulidhibiti viwavijeshi baada ya mamlaka kutoa lita za viuatilifu 81, 563 na kusambazwa katika halmashauri 57 za mikoa ya Lindi, Pwani, Morogoro, Geita, Manyara na Kilimanjaro. "Lita 561 za aina mbili za viuatilifu pia zilisambazwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa. Vilevile, wakulima 2,987 na maofisa ugani 16 katika Halmashauri ya Kilombeo, walipata mafunzo ya namna ya kudhibiti visumbufu vya mimea.

Mbali na viuatilifu, Prof. Ndunguru, alisema TPHA ilifanya ukaguzi wa mazao wa tani zaidi ya milioni 5.343 za nafaka za mizizi mbalimbali mipakani, bandarini na viwanja vya ndege na kutoa vyeti 29,033 vya usafirishaji wa mimea.





## Viongozi AMCOS wajengewa uwezo uzalishaji kahawa

**Na Timothy Itembe,** MARA

BODI ya Kahawa nchini imetoa mafunzo kwa viongozi wa Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) Mkoa wa Mara juu ya uzalishaji wa zao hilo lenye ubora kwa lengo la kuendelea kulinda soko.

Akieleza juu ya tatizo la ubora wa zao hilo nchini, Ofisa Msimamizi wa Ubora wa zao hilo Mkoa wa Mara, Anastaria Shirima alisema bado kahawa ipo chini katika ubora wa kimataifa.

Alisema imewalazimu kuwafikia wakulima, lengo likiwa ni kuhakikisha wanapata elimu juu ya uzalishaji wenye viwango vya ubora unaohitajika ili kuuzwa kwa bei nzuri.

Shirima alisema kuna haja wakulima kuondokana na kilimo cha mazoea na kufuata maelekezo ya wataalamu ili kupata maandalizi mazuri ya zao hilo ikiwa ni pamoja na uandaaji wa mavuno yaliyo bora na kupata fedha nyingi wakati wa kuuza sokoni.

"Kuna hatua zinazotakiwa kufuata ikiwa ni pamoja na kupanda kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu, kupalilia na kuweka mbolea kwa mjibu wa wataalamu, suala la muhimu zaidi ni kuzingatia uchumaji wa zao hili kwa kuchuma mbegu zilizokomaa zenye rangi nyekundu na siyo zenye rangi ya kijani," alisema.

Meneja Mkuu wa Chama cha Ushirika Mara (WAMACU), Samweli Gisoboye alisema wanamkakati wa kutoa miche kwa wakulima ikiwa ni moja ya hatua za kuongeza idadi ya wakulima kuwa wengi pamoja na kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Alisema kuwa chama hicho kina mpango wa kusimika mtambo wa kukoboa kahawa wenyewe ambao utakamilika haraka na wakulima kuondokana na kero ya kwenda kukoboa kwenye mashine za kampuni zingine zinazowalipisha bei kubwa.

# Halmashauri Maswa kutumia bil.7/- utekelezaji wa miradi

**Na Alex Sayi,** MASWA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu imepokea Sh.bilioni 7.08 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa halmashauri mpya.

Hayo yamebainishwa juzi na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Simon Berege wakati akizungumza na Nipashe, kueleza kuwa miradi mingine itakayotekelezwa ni katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na elimu, afya na miundombinu ya barabara.

Berege alisema ujenzi wa halmashauri hiyo itajengwa eneo la Ng'hami, utakaghalimu Sh.bilioni moja.

"Tumepokea Sh.bilioni moja kwa ujenzi wa halmashauri mpya maeneo ya Ng'hami, Sh.milioni 550 ununuzi wa vifaa tiba katika vituo vinne vya afya maeneo ya Zebeya, Shishiyu, Ipililo na Badi pamoja na zahanati nne eneo la Mwatumbe, Mwabayanda 'M',Njia panda na Isulilo."alisema Berege.

Aliongeza kuwa katika sekta ya elimu msingi na sekondari wamepokea zaidi ya Sh.bilioni 2.6 kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya katika Kijiji cha Mwabaratulu, ujenzi wa shule mpya mbili katika Kijiji cha Ilobi na Shishiyu sambamba na ujenzi wa madarasa 12.

"Tunaendelea na ukamilishaji wa madarasa 13, ofisi moja, Shule ya Msingi Hinduki, Mwasita, Nghaya, Masanwa, Masele, Maswa, Mwabuki, Mwafa, Mwanundi, Mbaragane na Mwashegeshi.

Alisema pia itahusisha ujenzi wa matundu ya vyoo zaidi ya 169 katika shule za msingi 18.

Berege alisema serikali Sh.mil 760 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 33 katika shule za sekondari 15 pamoja na ujenzi wa bweni katika Shule ya Sekondari Mwagala. "Kadhalika zipo fedha za TASAF zaidi ya Sh.milioni 930 zimetumika katika ujenzi wa bweni katika Shule ya Sekondari Budekwa, madarasa siata na matundu ya vyoo 18 katika Shule ya Msingi Mwabujiku, Mwawayi na Sangamwampuya pamoja na ujenzi wa miradi mingine ikiwemo zahanati mbili, nyumba nne za watumishi," alisema Berege.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Maswa, Grace Tungaraza alisema kuwa miradi ya TASAF imegawanyika katika makundi matatu.




Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi (wa pili kulia), akikagua gari la wagonjwa ambalo limenunuliwa na wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu katika Machimbo ya Mwakitolyo namba tano wilayani humo, mapema wiki hii. **PICHA: MARCO MADUHU**

# 10,000 wapewa elimu ya kudhibiti ukatili wa kijinsia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

WATU 10,000 kutoka katika makundi ya wanawake na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano wamepatiwa elimu ya kukabiliana na kudhibiti ukatili wa kijinsia, madhara na njia sahihi za kutoa taarifa ya vitendo hivyo.

Haya yalielezwa juzi na Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Kimataifa la watu wa Korea (KOICA), Heo Eun wakati wa hafla ya uzinduzi wa Kituo Jumuishi cha Waathirika wa Matukio ya Ukatili (SHUFAA) kilichopo Kata ya Bugarama. Alisema mradi huo ulikuwa wa miaka mitatu, umekamilika na kukabidhiwa rasmi serikalini kwa ajili ya utekelezaji na kusimamia yale yote yaliyokusudiwa ili kupambana na matukio hayo ambayo yanawaathiri kwa kiasi kikubwa watoto na wanawake nchini.

Aidha, alisema wanawake na watoto hao waliofikiwa ni kutoka katika Kata ya Bugarama Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga na Ikungi mkoani Singida, hivyo kila aliyefikiwa atakuwa akitoa taarifa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi ili kukomesha vitendo hivyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Fussi Mwageni alisema kwa asilimia kubwa mradi huo umesaidia katika kudhibiti vitendo vya ukatili wa kijinsia vilivyokuwepo na kutoa fursa kwa wanawake na watoto kwa kuwawezesha kiuchumi na sasa wanawake wanashughuli za kujiingia kipato.

Hata hivyo alisema jumla ya vikundi 60 vya wanawake na mabinti balehe vimepewa mafunzo ya ujasiriamali ili kuzalisha kwa tija na kuachana na utegemezi, kwamba wamepata gari ambalo watalitumia kuwafikia na kuwakumbusha madhara ya vitendo vya ukatili.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita aliwataka watoa huduma kwenye kituo hicho kutojihusisha katika vitendo vya rushwa wakati wa utaoaji wa haki kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia na badala yake wafanye kazi kwa kuzingatia miongozi na kuwa wasiri pale wanapopatiwa taarifa.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

# HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA DKT. ANGELINE S.L. MABULA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YAMAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24



MHE. DKT. ANGELINE S.L. MABULA (MB.)
WAZIRI

MHE. GEOPHREY MIZENGO PINDA (MB.)
NAIBU WAZIRI

ENG. ANTHONY D. SANGA
KATIBU MKUU

BI. LUCY D. KABYEMERA
NAIBU KATIBU MKUU

JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA DKT. ANGELINE S.L. MABULA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YAMAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24

**UTANGULIZI**

1. Mhe. Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua na kujadili Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03), naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka 2022/23. Naomba pia Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu hayo mawili kwa mwaka 2023/24.

2. Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa 11 wa Bunge la 12 ambalo ni mahsusi kwa ajili ya kujadili Mpango na Bajeti ya Serikali. Kwa heshima na taadhima naomba kutumia fursa hii kipekee kumshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuendelea kusimamia majukumu ya Sekta hii muhimu ya Ardhi. Nimuahidi na kum- hakikishia Mhe. Rais kwamba, imani aliyoionesha kwangu nitaendelea kuitafsiri kwa vitendo kwa kuhakikisha masuala muhimu yanayohusu ustawi na uendelevu wa Sekta hii yanasimamiwa na kutekelezwa ipasavyo kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

3. Mhe. Spika, kwa namna ya pekee, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais; Mhe. Dkt. Hus- sein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu na Mbunge wa Ruangwa kwa uongozi wao mahiri. Nawashukuru pia kwa miongozo, maelekezo na ushirikiano wao unaoniwezesha kutekeleza majukumu niliyokabidhiwa ya kuongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Katika kipindi cha miaka miwili umeleta mageuzi katika mifumo ya utoaji huduma, kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji, kuimarisha Sekta ya Milki na miradi mikubwa ya kuendeleza Sekta ya Ardhi.

4. Mhe. Spika, nawapongeza wewe binafsi, Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Najma Murtaza Giga Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Mhe. David Mwakiposa Kihenzile Mbunge wa Mufindi Kusini kwa kwa kuongoza shughuli za Bunge kwa umahiri na umakini.

5. Mhe. Spika, natoa pole kwako, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na wananchi wa Jimbo la Amani kwa kuondokewa na Mhe. Mussa Hassan Mussa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani-Zanzibar.

   Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema, Amina.

6. Mhe. Spika, napenda kuwapongeza Mhe. Timotheo Paul Mzava (Mb), kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb), kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati. Wizara inaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu ya usimamizi wa Sekta ya Ardhi.

7. Mhe. Spika, vilevile, nawapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri na Viongozi wengine walioteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika mabadiliko ya kiutendaji yaliyofanywa na Mhe. Rais hivi karibuni. Pia, nampongeza Mhe. Abdul Yussuf Maalim kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Amani

8. Mhe. Spika, napenda kuwapongeza Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb), kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhandisi Anthony Damian Sanga kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu na Bi. Lucy Dominico Kabyemera kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii.

9. Mhe. Spika, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa uchambuzi na ushauri iliyoutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kwa mwaka 2023/24.

   Wizara inalihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa itaendelea kuzingatia maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati katika kuboresha utendaji kazi ili kuongeza tija katika utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi.

10. Mhe. Spika, nawashukuru wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kwa kura nyingi zilizopelekea kuchaguli- wa kwangu kuwa mjumbe wa NEC. Pia nawashukuru viongozi wa CCM kwa miongozo, ushauri na maelekezo mbalimbali wanayonipatia kuhakikisha Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2020 inatekelezwa kwa ufanisi. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Ilemela kwa ushirikiano wanaonipa wakati ni- kitimiza majukumu yangu kama mwakilishi wao hapa Bungeni. Kipekee kabisa, naishukuru sana familia yangu kwa kuwa karibu nami na kuendelea kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu. Kadhalika, na- washukuru viongozi wa dini kwa sala na dua ambazo zinanipa nguvu katika kutekeleza majukumu yangu.

11. Mhe. Spika, baada ya maelezo ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango na Ba- jeti ya Wizara kwa mwaka 2022/23 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/24. Bajeti hii imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); Mikataba; Itifaki; Mipango na Makubaliano mbalimbali ya kikanda na kimataifa; Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Sekta ya Ardhi na Kitaifa; na maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

**UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2022/23 NA MALENGO YA MWAKA 2023/24.**

**Matumizi**

12. Mhe. Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 105.5. Aidha, Wizara iliongezewa bajeti ya shilingi bilioni 69.8 ikiwa ni fedha za ndani za Maendeleo na kulipa madeni. Ongezeko hilo limefanya bajeti ya Wizara kufikia shilingi bilioni 175.3. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara imepokea jumla ya shilingi bilioni 147.7 kati ya bajeti ya shilingi bilioni 175.3 sawa na asilimia 84.2 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni 21.5 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ya Wizara na Taasisi sawa na asilimia 64 ya bajeti ya OC; shilingi bilioni 32.8 ni mishahara ya watumishi sawa na asilimia 74 ya bajeti ya mshahara; na shilingi bilioni 93.3 ni fedha za maendeleo sawa na asilimia 96.1 ya bajeti yote ya miradi ya maendeleo. (Jedwali Na. 1).

13. Mhe. Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara kupitia Fungu 48 ilipanga kukusanya shilingi bilioni 250.1 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ya Sekta ya Ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara ime- kusanya shilingi bilioni 133 sawa na asilimia 53.2 ya lengo (Jedwali Na.2).

14. Mhe. Spika, ili kufikia lengo la makusanyo, Wizara inaendelea kuboresha kumbukumbu na mifumo ya TE- HAMA iliyopo ili iweze kutuma ujumbe kwa njia ya simu. Maboresho hayo yamewezesha kutuma ujumbe mfupi wa kuwakumbusha kulipa kodi ya pango la ardhi wamiliki 202,563 katika kipindi cha Februari-Mei, 2023. Utarati- bu huu ni endelevu. Aidha, Wizara imetumia taarifa za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 kuhuisha kumbukumbu za wamiliki na pia kutambua vipande vya ardhi 524,131 katika maeneo yasiyopangwa na kuviingi- za kwenye kanzidata kwa lengo la kuongeza wigo wa ma- kusanyo.

15. Mhe. Spika, Katika kujenga mazingira rafiki ya kuwezesha wananchi kuitikia wito wa kulipa kodi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa msamaha wa kulipa deni la msingi bila riba kwa kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Aprili 2023. Kupitia msamaha huo jumla ya shilingi bilioni 38 imelipwa na wamiliki 15,986 ikiwa ni madeni ya msingi, na kiasi cha shilingi bilioni 27 ikiwa ni riba kimesamehewa.

16. Mhe. Spika, kwa mwaka 2023/24, Wizara imeweka lengo la kukusanya shilingi bilioni 300 kwa kupitia mikakati iliyojiwekea ikiwemo kuhuisha na kutunza kumbukumbu za wamiliki wa ardhi katika mfumo wa kielektroniki ili kurahisisha utumaji wa ankara kwa kutumia simu za viganjani; kuimarisha miundombinu ya TEHAMA; kutoa elimu; kuhuisha viwango vya ukadiriaji kodi; na kuhamasisha Halmashauri na Sekta binafsi kuendelea kupima na kumilikisha maeneo mapya ili kuongeza wigo wa makusanyo.

    Natoa rai kwa wamiliki wote wa ardhi nchini kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati kama sehemu ya mchango wa maendeleo ya Taifa letu lakini pia kuepuka usumbufu endapo watachukuliwa hatua za kisheria kwa ukiukaji wa sheria, kanuni na tarati- bu.

**MAPATO NA MATUMIZI YA FUNGU NA.03**

17. Mhe. Spika, katika mwaka 2022/23, Tume iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 8.9. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Tume imepokea jumla ya shilingi bilioni 5.97 kati ya bajeti ya shilingi bilioni 8.9 sawa na 67.4% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 1.1 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) sawa na 70.6% ya bajeti; shilingi 1.95 ni Mishahara sawa na 98.8%; na shilingi 2.97 ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Maendeleo sawa na 55.0%.

**UTAWALA WA ARDHI**

18. Mhe. Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 74(a) ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 inaelekeza kuhusu kuhakikisha ardhi yote inapangwa, kupimwa na kumilikishwa kwa wananchi kwa manufaa ya kiuchumi na kijamii. Kwa kuzingatia maelekezo haya katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kuandaa Hatimiliki 500,000, Hati za Hakimiliki za Kimila 520,000 na Hati za Sehemu ya Jengo 1,000. Aidha, Wizara iliahidi kusajili miamala ya hatimiliki na Nyaraka za Kisheria 100,000 na kutoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji 100. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara imeandaa na kusajili Hatimiliki 76,746 sawa na asilimia 15.3 ya lengo. Jumla ya Hati za Hakimiliki za Kimila 51,762 zimetolewa sawa na asilimia 10 ya lengo (Jedwali Na.3). Hatimiliki hizi zimeleta ti- ja katika uchumi wa wananchi na taifa kwa ujumla.

    Hadi tarehe 15 Mei, 2023 mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni 60.1 imetolewa na Taasisi za fedha kwa kutumia Hati za Hakimiliki za Kimila 1,382 katika Wilaya za Mbozi, Iringa, Babati, Bariadi, Arumeru, Mbarali, Manyoni, Kilombero, Bagamoyo, Mbinga na Tandahimba. Napenda kuwahakikishia wananchi na Taasisi za fedha kuwa Hati za Hakimiliki za Kimila ni nyaraka halali za kisheria hivyo, nasisitiza waendelee kuzitumia kwa man- ufaa ya kiuchumi.

19. Mhe. Spika, Wizara haikuweza kufikia malengo kati- ka uandaaji na usajili wa Hatimiliki na Hati za Hakimiliki za Kimila kutokana na kuchelewa kuanza kwa mradi wa Uboreshaji wa usalama wa Milki za Ardhi, kutokamilika kwa wakati miradi ya KKK katika mamlaka za upangaji, wananchi wengi kutokamilisha ulipaji wa gharama za umilikishaji na changamoto ya mifumo ya TEHAMA.

20. Mhe. Spika, katika mwaka 2023/24, Wizara itaan- daa na kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila 520,000, Hat- imiliki 500,000 na Hati za Sehemu ya Jengo 1,000. Vilevile, Wizara itasajili miamala ya Hatimiliki na Nyara- ka za kisheria 100,000. Wizara inatarajia kufanikisha malengo haya kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Miliki za Ardhi, Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK), na Mradi wa Kuboresha Miundombinu ya Upimaji na Ramani kwa kushirikisha wadau wa sekta binafsi, kuimarisha mifumo ya TEHAMA ambayo itarahisisha utoaji wa Hatimilki na kupitia upya viwango vya tozo na ada za umilikishaji ili kuleta unafuu kwa wananchi.

**ARDHI YA UWEKEZAJI**

21. Mhe. Spika, Wizara kupitia Kamati ya Taifa ya Uga- waji Ardhi inasimamia uidhinishaji wa maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Vikao vinne (4) vya Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji wa Ardhi vilipokea na kupitisha maombi 135 ya ardhi yaliyowasilishwa yenye ukubwa wa hekta 29,820.4 zilizoombwa kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje (Jedwali Na. 5).

    Uwekezaji huu una mtaji wa thamani ya dola za Marekani milioni 3.4 sawa na shilingi Trilioni 7.8 za Tanzania. Katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kuratibu ugawaji na usimamizi wa maeneo ya ardhi ya uwekezaji.

22. Mhe. Spika, Wizara inaendelea kuhuisha kumbukumbu na kuziingiza katika Mifumo ya TEHAMA ili kuwezesha utoaji wa huduma kwa urahisi na muda mfupi. Aidha, uhakiki unafanyika kwa kutumia taarifa zilizokusanywa katika zoezi la anuani za makazi na sen- sa ya watu na makazi pamoja na kumbukumbu za vi- wanja husika.

    Ninaishukuru Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kwa kubuni mfumo wa NaPA (National Physical Addressing System) ambao umewezesha kupatikana kwa taarifa zinazotumika katika kurahisisha uhuishaji wa kumbukumbu za wamiliki wa ardhi. Mfumo huo utasaidia ukusanyaji na ufuatiliaji wa kodi ya pango la ardhi kwa kutumia majira ya nukta na usimamizi wa uendelezaji wa miji.

23. Mhe. Spika, hadi 15 Mei 2023 Wizara imehuisha kumbukumbu za wamiliki wa ardhi 635,833 kati y 500,000 zilizopangwa kuhuishwa kufikia Juni 2023 sawa na asilimia 127 ya lengo. Zoezi hili linatekelezwa kwa kutumia wataalam kutoka Serikalini na wataalam wa muda 26.

    Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza kwa kazi kubwa na ya kizalendo ambayo imewezesha uchakataji kidigitali wa taarifa hizo. Katika mwak 2023/24, Wizara itaendelea na zoezi la kuhuisha kumbukumbu za ardhi.

**UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI KIUTAWALA**

24. Mhe. Spika, Katika kutekeleza Ibara ya 74(i) ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Wizara imeendelea kushughulikia migogoro ya ardhi kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo madawati ya kushughulikia malalamiko, kliniki za ardhi, Kamati Maalum ya Wataalam wa Wizara na ziara za viongozi katika maeneo mbalimbali nchini.

    Vilevile, Wizara imeendelea kupanga matumizi ya ardhi na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 migogoro 2,684 imeshughulikiwa kiutawala (Jedwali Na. 6). Kadhalika, Wizara imeendelea kuhuisha rejista za migogoro katika ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri ili kuwa na taarifa za migogoro ambayo inaendelea na utatuzi na iliyopatiwa ufumbuzi ili kuepuka kujirudia. Katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kushughulikia migogoro ya ardhi kadri itakavyokuwa ikijitokeza.

**UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI KATIKA JIJI LA DODOMA**

25. Mhe. Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na mamlaka zingine za Serikali iliunda Kamati ya wataalam kushughulikia kero na malalamiko ya wananchi hususani katika Mikoa yenye migogoro mingi kwa ikiwemo Dodoma.

26. Mhe. Spika, Kwa Jiji la Dodoma, jumla ya migogoro 815 ilipokelewa ambapo migogoro 429 sawa na asilimia 52.6 ilipatiwa ufumbuzi na migogoro 386 inaendelea kushughulikiwa. Vyanzo vya migogoro iliyobainika ni pamoja na uwepo wa milki pandikizi, madai ya fidia, wananchi kutoridhika na upimaji shirikishi, uwepo wa watumishi wengi wa kujitolea waliokosa





uratibu na usimamizi wa karibu na uzingatiaji hafifu wa sheria na taratibu zinazoongoza Sekta ya Ardhi na ukosefu wa maadili kwa baadhi ya watumishi.

27. Mhe. Spika, Katika utekelezaji wa mapendekezo ya kumaliza migogoro iliyopo Wizara iliamua kuchukua hatua za haraka kwa kuwaondoa watumishi wote wa muda katika Jiji la Dodoma ili kudhibiti migogoro iliyokuwa inaendelea kuzalishwa. Katika mwaka 2023/24, Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali itaendelea na utaratibu wa kutatua migogoro katika mikoa yenye migogoro mingi ikiwemo Mikoa ya Arusha, Mwanza, Mbeya na Morogoro.

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Katika Vijiji 975**

28. Mhe. Spika, Kamati ya Mawaziri wa Kisekta inayorat- ibu utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusu migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji 975 nchini inaendelea kusimamia utekelezaji wa uamuzi huo katika mikoa mbalimbali. Hadi tarehe 15 Mei, 2023, Kamati ya Mawaziri imefanya ziara kwenye mikoa yote 26. Kazi zilizotekelezwa na Kamati hiyo ni pamoja na kutoa mat- amko kuhusu uamuzi wa Baraza la Mawaziri, kufanya vikao na viongozi wa ngazi mbalimbali na kuweka mika- kati ya utekelezaji katika ngazi ya mkoa kwa ku- shirikiana na timu ya wataalam wa kisekta.

29. Mhe. Spika, kazi zinazoendelea kutekelezwa na timu ya wataalam wa kisekta kwa wakiongozwa na Wakuu wa Mikoa ni pamoja na kubainisha maeneo yatakayomegwa na kutolewa kwa wananchi; kutafsiri mipaka ya baadhi ya hifadhi na kuweka alama za kudumu na zinazoon- ekana ardhini; kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwenye vijiji vinavyopakana na Hifadhi za Taifa; na kufanya tathmini na uthamini kwa wananchi wa- takaopisha shughuli za uhifadhi kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Serengeti (Ghuba ya Speke).

30. Mhe. Spika, katika kutekeleza maamuzi ya Serikali, ardhi yenye ukubwa wa ekari 2,385,316 imetolewa kwa wananchi baada ya kumegwa au kufutwa kwa baadhi ya maeneo ya Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Hifadhi za Misitu.

Maeneo hayo yanaendelea kuandaliwa mipango ya ma- tumizi ya ardhi ili yaweze kutumika kwa ajili ya shughuli za makazi, kiuchumi na kijamii.

31. Mhe. Spika, utatuzi wa mgogoro wa mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha unaotokana na Tangazo la Serikali Na. 28 la mwaka 2008 (GN 28) unaogusa Wilaya za Mbarali na Chunya unaendelea chini ya uratibu wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Kazi ya marekebisho ya mpaka uwandani imekamilika ambapo alama 671 za kudumu zinazoonekana kirahisi zimewekwa katika eneo lenye urefu wa kilomita 344 na mkuza wenye urefu wa kilomita 177 umechongwa. Aidha, marekebisho ya Tangazo la Serikali (GN 28) yako katika hatua za ukamilishaji.

32. Mhe. Spika, katika kutekeleza zoezi hilo jumla ya ekari 854 kati ya 1,500 zimepatikana katika vijiji vya Uhambule, Chamoto, Nyamakuyu, Iheha, Nyakadete, Mapogoro, Nyakazombe na Miyombweni kwa ajili ya makazi ya wananchi watakaopisha maeneo ya hifadhi. Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeandaliwa katika Vijiji 15 kati ya 23 vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Kazi ya uthamini kwa ajili ya fidia imefanyika kwa wananchi 4,072 katika vijiji vinne (4) vya Kilambo, Iyala, Masundasi na Msanga kati ya vijiji vitano (5) na kazi hiyo inaendelea katika Kijiji cha Luhanga na vitongoji 15 kati ya 38 vilivyopo katika vijiji 16 Wilayani Mbarali.

Napenda kuwashukuru wakuu wa Mikoa, Wabunge na Wataalam wote kwa ushirikiano wao wakati wa utekelezaji wa zoezi.

**MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA**

33. Mhe. Spika, Katika mwaka 2022/23, Wizara imefa- nikiwa kuongeza idadi ya Mabaraza Mabaraza mapya 12 ambayo yameanza kutoa huduma na hivyo kuwa na jumla ya Mabaraza 92 yanayotoa huduma kati ya Maba- raza 139 yaliyoanzishwa. Kuanzishwa kwa mabaraza ha- yo kumepunguza muda wa kusafiri na gharama kwa wananchi katika maeneo husika.

Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 mashauri 23,412 kati ya 33,250 sawa na 70% ya lengo yalitolewa maamuzi na mashauri 15,710 yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, katika mwaka 2023/24, Wizara inatarajia kufungua mabaraza mapya 47.

**UTHAMINI WA MALI**

34. Mhe. Spika, Katika mwaka 2022/23, Wizara ilipanga kuratibu uandaaji na uidhinishaji wa taarifa za uthamini 54,000 ambazo kati ya hizo, uthamini wa kawaida 20,000 na taarifa za wafidiwa 34,000 na kushughulikia migogoro 30 ya uthamini wa fidia. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara imeidhinisha taarifa za uthamini 61,211 sawa na asilimia 113 ya lengo ambapo kati ya taarifa hizo, uthamini wa kawaida 21,272 na taarifa za wafidiwa 39,939. Aidha, migogoro 20 ya fidia imepoke- lewa na kushughulikiwa.

35. Mhe. Spika, Katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kuboresha kanzidata ya viwango vya thamani ya ardhí, mazao na kuhuisha viwango vya kodi ya ardhí nchini ili kuhakikisha uthamini unafanyika kwa kuzingatia bei ha- lisi ya soko na hivyo kuwezesha ulipaji wa fidia stahiki, kupunguza malalamiko kutoka kwa wananchi na kuiwezesha Serikali kupata kodi stahiki. Napenda kulia- rifu Bunge lako Tukufu kuwa viwango vya thamani ya ardhi na mazao vimehuishwa na vimeanza kutumika kuanzia mwezi Aprili, 2023. Wizara itahakikisha viwango hivi vinatumika kwa usahihi na kwa kuzingatia sheria na taratibu za uthamini ili kuhakikisha wananchi wanalip- wa fidia stahiki inayoendana na bei ya soko.

36. Mhe. Spika, Katika kipindi mwaka 2022/23, Wizara imeshiriki na kuratibu mazoezi mbalimbali ya uthamini kwa ajili ya fidia kwa wananchi wanaopisha miradi mbalimbali ya Serikali inayoendelea pamoja na wananchi wanaopisha maeneo ya hifadhi (Jedwali Na.7).

37. Mhe. Spika, Katika mwaka 2023/24 Wizara itaratibu na kusimamia uandaaji wa taarifa za uthamini 54,000, kati ya hizo, uthamini wa kawaida 20,000 na uthamini wa fidia wenye wafidiwa 34,000. Vilevile, Wizara itaende- lea kushughulikia malalamiko yatokanayo na uthamini wa fidia, na kuendelea kuratibu utekelezaji wa mazoezi mbalimbali ya uthamini wa fidia katika miradi inayote- kelezwa na Serikali.

38. Mhe. Spika, matumizi ya TEHAMA ni muhimu katika sekta ya Ardhi kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 74(b) ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Kwa kuzingatia maelekezo haya Wizara inaendelea kukamilis- ha maboresho ya Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (Integrated Land Management Information System – ILMIS) kwa kutumia watalaam wa ndani. Aidha, pamoja na maboresho yanayoendelea, mfumo huu umeendelea kutumika katika kutoa hati za kielektroniki katika Jiji la Dodoma na Mkoa wa Dar es Salaam. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 jumla ya hati za kielektroniki 23,150 zimetolewa kupitia mfumo huo na kufanya hati zote za kielektroniki zilizotolewa kuwa 55,550.

39. Mhe. Spika, katika hotuba ya bajeti ya Mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kujenga, kusimika na kuimarisha miundombinu wezeshi ya TEHAMA kwa awamu katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri nchini na kukarabati mtandao kiambo katika ofisi za ardhi za halmashauri 47 zikiwemo makao makuu ya mikoa ya Iringa, Lindi, Mwanza na Mbeya.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara imekamilisha kujenga miundombinu wezeshi katika ofisi za ardhi za halmashauri za Wilaya ya Chalinze, Chamwino na Mkuranga. Vilevile, Wizara imekamilisha kujenga mtandao kiambo (Local Area Network) katika ofisi za ardhi za mikoa ya Iringa, Lindi, Mwanza na Mbeya na kuiunganisha na Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi (National Land Information Centre-NLIC).

Aidha, Wizara inakamilisha usimikaji wa mtandao kiambo katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri 44.

40. Mhe. Spika, Katika mwaka 2023/24, Wizara inatarajia kusimika na kusambaza miundombinu ya mtandao kiambo katika ofisi za ardhi za mikoa 26 na halmashauri 132 na hivyo kuwezesha kukamilisha usambazaji wa mfumo wa ILMIS katika halmashauri zote nchini. Vilevile katika mwaka 2023/2024, Wizara itaanzisha wavuti ya wateja (self-service portal) ambapo mwananchi atapata huduma kupitia wavuti hiyo bila kulazimika kwenda ofisi za ardhi. Kupitia huduma hii, mwananchi atakuwa na uwezo wa kufuatilia kila hatua ya maombi kwa njia ya simu ama huduma ya mtandao.

Ubadilishaji wa Michoro ya Mipangomiji, Ramani za Upimaji na Nyaraka za Umiliki Kutoka Analogia Kwenda Digitali

41. Mhe. Spika, Wizara katika mwaka 2022/23, iliahidi kubadilisha taarifa za ardhi kutoka mfumo wa analogia kwenda kidigitali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 michoro ya mipangomiji 30,812 yenye jumla ya viwanja 7,241,686 na ramani za upimaji 112,297 zenye jumla ya viwanja 2,385,114 zimebadilishwa katika mikoa yote 26. Vilevile, nyaraka za Hati na majalada 524,131 yamebadilishwa kwa asilimia 100 katika ofisi za ardhi za mikoa 15 ya Kagera, Geita, Rukwa, Katavi, Songwe, Tabora, Dodoma, Singida, Shinyanga, Mbeya, Njombe, Kigoma, Iringa, Simiyu na Manyara.

42. Mhe. Spika, katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea na zoezi la ubadilishaji wa taarifa za ardhi kutoka mfumo wa analojia kwenda kidigitali kwa nyara- ka za Hati na majalada 1,647,326 katika ofisi za ardhi za mikoa 11 ya Dar es Salaam, Mwanza, Kilimanjaro, Mtwara, Arusha, Pwani, Lindi, Mara, Morogoro, Ruvuma na Tanga na mamlaka za Serikali za Mitaa.

**UPANGAJI MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI**

43. Mhe. Spika, Wizara katika mwaka 2022/23, iliahidi kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji katika uandaaji na utekelezaji wa Mipango Kabambe kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo na kwa kuzingatia Ibara ya 74(a) ya Ilani ya CCM. Hadi tarehe 15 Mei, 2023, Mpango Kabambe mmoja (1) wa Manispaa ya Moshi umekamilika na kuidhinishwa. Rasimu za Mipango Kabambe miwili (2) ya miji ya Mafinga na Bagamoyo ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji na Mipango Kabambe ya Manispaa ya Kahama na Mji wa Chalinze ipo katika hatua za awali za utayarishwaji.

Aidha, katika kipindi hicho Wizara imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mipango katika Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya, na Manispaa za Morogoro, Lindi, Mtwara Mikindani na Songea.

Ufuatiliaji huo ulibaini changamoto za utekelezaji kwa baadhi ya halmashauri kuandaa mipangokina na utoaji wa vibali vya ujenzi inayokinzana na Mipango Kabambe. Kufuatia changamoto hizo, Wizara imezielekeza halmas- hauri kuzingatia Mipango Kabambe iliyoandaliwa wakati wa usanifu wa mipangokina na utoaji wa vibali vya ujen- zi.

44. Mhe. Spika, katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Mipango Kabambe katika Halmashauri sita (6) za Majiji ya Tanga na Arusha, Manispaa ya Moshi na Miji ya Korogwe, Kibaha na Babati. Vilevile Wizara itafuatilia utayarishaji wa Mipango Kabambe minne (4) na kuratibu uandaaji wa Mipango kabambe sita (6) katika Halmashauri za miji ya Kasulu, Masasi, Bunda, Mbinga, Nzega na Mbozi. Natoa rai na kuzihimiza Mamlaka za Upangaji nchini kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji, utekelezaji na udhibiti uendelezaji miji ili kuwezesha miji yetu kusanifiwa na kuendelezwa kwa kuzingatia Mipango Kabambe.

45. Mhe. Spika, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kumekuwepo na ongezeko kubwa la ukuaji wa miji na kusababisha hitaji kubwa la kubadilisha matumizi ya ardhi ili kukidhi mahitaji. Katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kuratibu uidhi- nishaji wa maombi 300 ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi ambapo hadi tarehe 15 Mei, 2023, jumla ya maombi 611 sawa na asilimia 204 ya mabadiliko ya ma- tumizi ya ardhi yaliidhinishwa.

Hivyo, Wizara imetoa maelekezo kwa Ofisi za ardhi za Mikoa na Halmashauri kufanya ukaguzi ili kubainisha maeneo yote yaliyobadilishwa matumizi kinyume cha utaratibu na kuchukua hatua za kisheria kwa wahusika ikiwemo kutoza asilimia 2 ya thamani ya maendelezo yaliyofanyika kinyume cha utaratibu.

46. Mhe. Spika, katika kuhakikisha udhibiti wa ukuaji holela wa vijiji vinavyochipukia kuwa miji, Wizara ime- sambaza Mwongozo wa Upangaji na Ujenzi wa Nyumba Bora Vijijini ulioboreshwa kwa lugha ya picha kurahisis- ha utekelezaji wake katika vijiji. Mwongozo huo utasaidia kuongoza utengaji wa maeneo ya huduma za jamii na za kiuchumi katika vijiji na kuboresha upangaji wa vijiji na hatimaye kuwa na miji iliyopangika vizuri, endelevu na nyumba bora.

Halmashauri za vijiji pamoja na majukumu mengine zi- takuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa Mwon- gozo nautungaji wa Sheria Ndogo za kulinda mipango na kuhakikisha zinazingatiwa. Ili kujenga uelewa wa mwon- gozo huo, Wizara imeanza kutoa elimu kwa umma kupi- tia viongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri katika mi- koa ya Mbeya, Morogoro, Geita, Mwanza na Dodoma na kazi hiyo inaendelea katika mikoa mingine. Kazi ya kusambaza na kutoa elimu kuhusu mwongozo huo ina- tarajiwa kukamilika katika mwaka 2023/2024. Aidha, Wizara itatangaza rasmi tarehe ya uzinduzi wa Mwongozo huu.

Usimamizi na Uratibu wa Sekta ya Nyumba

47. Mhe. Spika, Katika mwaka 2022/23, Wizara ilipanga kuwezesha kuboreshwa kwa mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kupitia Tanzania Mortgage Refinance Company (TMRC). Hadi tarehe 15 Mei, 2023, Serikali kupitia TMRC imewezesha taasisi za fedha 32 kutoa mikopo yenye riba nafuu kiasi cha shilingi bilioni 26.34 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Katika mwaka 2023/24, Wizara itaendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kutumia fursa za kupata mikopo ya ujenzi wa nyumba kutoka katika taasisi za fedha ambazo zinapokea fedha Serikalini kupitia TMRC.

48. Mhe. Spika, Katika mwaka 2022/23, Wizara imeendelea kuratibu upatikaji wa mikopo kwa watumishi kulingana na taratibu zilizowekwa. Hadi tarehe 15 Mei, 2023 watumishi 49 waliokidhi vigezo wamepatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 606.83 kati ya watumishi 99 waliotimiza masharti ya mkopo. Katika mwaka 2023/24, mfuko umepanga kukopesha watumishi 100.

**Sensa ya Majengo ya Mwaka 2022**

49. Mhe. Spika, Kwa kuzingatia matakwa Ibara ya 74(d) ya Ilani ya CCM, katika mwaka 2022/23 Wizara iliahidi kushiriki katika zoezi la kitaifa la Sensa ya Watu na Makazi ambalo lilihusisha pia ukusanyaji wa taarifa za majengo nchini.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba zoezi hilo limefanyika kwa mafanikio makubwa. Hivyo nichukue fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ambao walifanya kazi kwa juhudi katika kuhakikisha kuwa Sensa ya Majengo inatekelezwa kama ilivyopangwa. Kazi ya kuchakata taarifa zilizotokana na matokeo ya sensa ngazi ya Taifa imekamilika ambapo imebainishwa kuwa Tanzania Bara ina majengo milioni 13.9 kati ya hayo majengo milioni 4.1 sawa na asilimia 29.7 yapo mijini na majengo milioni 9,8 sawa na asilimia 70.3 yapo vijijini. Kati ya majengo hayo, majengo milioni 12.7 sawa na asilimia 91.4 ni ya makazi, majengo 470,476 sawa na asilimia 3.4 ni ya makazi na biashara na majengo 719,582 sawa na asilimia 5.2 ni majengo ya matumizi mengineyo.

50. Mhe. Spika, kati ya majengo yote, majengo ya kawaida ni milioni 13.2 sawa na asilimia 94.4, ya ghorofa ni 61,258 sawa na asilimia 0.4 na majengo 694,395 sawa na asilimia 5 ni majengo yaliyo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Matokeo haya yana mchango chanya katika kuiwezesha Wizara kupitia upya na kuboresha sera, miongozo na mikakati ya usimamizi wa ardhi na uendelezaji makazi mijini na vijijini. Majengo mengi yanajengwa kwa mtawanyiko hivyo kusababisha athari katika utoaji wa huduma za msingi kama vile afya, elimu, barabara, maji, umeme na upatikanaji wa maeneo ya umma na kupunguza maeneo ya hifadhi za misitu, ardhi ya malisho na ardhi inayofaa kwa kilimo.

**UPIMAJI ARDHI NA UANDAAJI RAMANI**

51. Mhe. Spika, Katika mwaka 2022/23, Wizara iliahidi kusimika alama mpya za msingi 100 katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023 alama za msingi za upimaji 106 zilisimikwa katika mikoa 10 ya Dodoma, Pwani, Iringa, Mbeya, Tanga, Manyara, Singida, Kagera, Geita na Tabora na hivyo kuwa na jumla ya alama za upimaji 1,041 nchini. Katika maeneo mengi nchini alama za msingi za upimaji zimewekwa katika umbali wa kilometa 40 kutoka alama moja kwen- da nyingine. Hali hii husababisha kuongezeka kwa gha- rama za upimaji na muda mrefu wa upimaji. Ili kukabil- iana na changamoto hii, Wizara imeendelea kusimika alama hizi ili kupunguza wastani wa umbali wa sasa hadi kufikia kilometa 20 kati ya alama moja na nyingine.

52. Mhe. Spika, katika mwaka 2023/24, Wizara itaanza hatua za awali kwa ajili ya ujenzi wa vituo 22 vya upimaji (Continuously Operating Reference Station- CORS) vinavyofanya kazi muda wote yaani mchana na usiku katika makao makuu ya mikoa 22 (Jedwali Na. 10A) na pia itasimika alama mpya za msingi 276 katika Halmashauri 25 za mikoa 10 (Jedwali Na. 10B).

**Upimaji wa Ardhi**

53. Mhe. Spika, Katika mwaka 2022/23, Wizara kwa kushirikiana na wadau zikiwemo mamlaka za upangaji ilipanga kuratibu upimaji na uidhinishaji wa ramani za viwanja na mashamba 500,000.

Hadi tarehe 15 Mei, 2023, viwanja 314,977 na mashamba 2,564 yalipimwa na kuidhinishwa na kutunzwa kwenye kanzidata ya Wizara sawa na asilimia 63 ya lengo (Jedwali Na.11). Katika mwaka 2023/24, Wizara itasimamia upimaji na uidhinishwaji wa viwanja 500,000 na mashamba 500.


**MIRADI YA MAENDELEO Mradi wa KKK.**

54. Mhe. Spika, katika kutekeleza Ibara ya 74(f) ya Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 mwaka 2021/22 Serikali ilizikopesha Halmashauri 57, Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa, Vyuo vitatu vya Ardhi vya Tabora, Morogoro na Chuo Kikuu cha Ardhi jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 50 ambapo utekelezaji wake uliendelea mwaka 2022/23. Pia, katika mwaka 2022/23 Wizara ilipokea Kiasi cha shilingi bilioni 10.6 kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ya KKK nchini.

Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, kazi zilizotekelezwa ni upimaji wa viwanja 116,499 na mashamba 401 sawa na asilimia 39 ya lengo la viwanja 300. Upimaji huo unafanya jumla ya viwanja vilivyopimwa kupitia fedha za mkopo wa Shilingi bilioni 50 kuwa viwanja 232,723.

55. Mhe. Spika, ili kuhakikisha fedha zilizotolewa zinarejeshwa, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango imeendelea na uratibu na ufuatiliaji marejesho ya fedha hizo katika Halmashauri 57 na Taasisi zilizopatiwa fedha hizo.

Kupitia ufuatiliaji huo, Halmashauri 48 zimerejesha jumla ya shilingi bilioni 17.2 ambapo Halmashauri tisa (9) na Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Iringa





zimerejesha kwa asilimia 100, Halmashauri 40 na vyuo vya Ardhi zimerejesha sehemu ya fedha na Halmashauri 8 hazijarejesha kabisa.

56. Mhe. Spika, nazipongeza Halmashauri za Jiji la Mwanza, Manispaa za Morogoro na Ilemela; Miji ya Tunduma na Bariadi; Halmashauri za Wilaya za Moshi, Meru, Geita, na Mbozi kwa kukamilisha marejesho ya fedha za mkopo. Hata hivyo, Halmashauri za Wilaya za Sumbawanga, Babati, Kishapu, Musoma, Mji wa Ifakara, Manispaa ya Shinyanga, Shinyanga DC na Chalinze DC hazijarejesha kabisa fedha za walizokopeshwa kutekeleza miradi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha ardhi (Jedwali Na.12 A, B, C na D). Aidha Natoa wito kwa Taasisi na Halmashauri ambazo hazijakamilisha marejesho kurejesha fedha hizo ndani ya muda uliowekwa na Serikali ili kuziwezesha Halmashauri nyingine kunufaika na fedha hizo kwa utaratibu endelevu.

57. Mhe. Spika, katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia mradi itaendelea kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi 300,000 kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji pamoja na Sekta Binafsi.

**Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP)**

58. Mhe. Spika, Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi unatekelezwa na Serikali kwa Mkopo toka Benki ya Dunia wa Dola za Kimarekani milioni 150 sawa na shilingi za kitanzania bilioni 345. Utekelezaji wa mradi huu umeanza rasmi mwaka 2022/2023 na utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2022/23 – 2026/27). Mradi umelenga kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Ardhi nchini kama zilivyoanishwa katika uk. 60 – 61 katika kitabu cha Hotuba.

59. Mhe. Spika, ili kutatua changamoto hizi, Mradi utatekeleza yafuatayo:
   i. Urasimishaji wa makazi yasiyopangwa;
   ii. Uboreshaji wa miundombinu ya usimamizi wa ardhi;
   iii. Kujenga ofisi za ardhi za mikoa na kukarabati ofisi za ardhi zilizopo Halmashauri;
   iv. Usimikaji, usambazaji na ufungaji wa unganishi wa kielektroniki (ILMIS); mfumo
   v. Ubadilishaji wa nyaraka kutoka analogia digitali; na kwenda
   vi. Utoaji wa vitendea kazi, kuwajengea uwezo watumishi ili kuimarisha utendaji. Takwimu za matokeo ya utekelezaji zinapatikana katika Uk. 61 – 62 wa kitabu cha Hotuba

**Utekelezaji wa mradi katika mwaka 2022/23 na ma- lengo ya mwaka 2023/24.**

60. Mhe. Spika, katika mwaka 2022/23, Wizara ilipanga kuanza kujenga majengo ya Ofisi za Ardhi za Mikoa 25; kuboresha mfumo wa ILMIS; kutoa Hatimiliki 500,000 katika Halmashauri 23; kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila 200,000 katika Vijiji 200 na kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 200 katika Wilaya sita (6) na kutoa Leseni za Makazi 250,000. Katika utekelezaji wa kazi hizi, Wizara ilitarajia kutoa ajira za muda mfupi 2,300 na vibarua 4,200.

61. Mhe. Spika, mpaka sasa usanifu wa majengo ya ofisi za ardhi za mikoa 25 umefanyika na zabuni imetangazwa na usimikaji wa alama za msingi za upimaji 67 umefanyika ili kuwezesha upimaji wa ardhi na utoaji wa Hatimiliki katika maeneo hayo.

62. Mhe. Spika, majaribio ya namna bora ya kuongeza kasi ya zoezi la urasimishaji kwa lengo la kutoa hatimiliki yanafanyika katika Jiji la Dodoma katika mitaa mitatu (3) ya Bihawana kata ya Mbabala; Mapinduzi B kata ya Ng'ongh'ona; na Mkwawa kata ya Mpunguzi. Maeneo ya mitaa hiyo yametambuliwa na michoro ya mipangomiji imeandaliwa. Njia mbalimbali zinafanyiwa majaribio ambapo njia itakayoonesha ufanisi itatumika katika maeneo mengine ya mradi. Katika utekelezaji wa kazi za mradi ajira za muda mfupi 1,200 zilipatikana.

63. Mhe. Spika, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, uandaaji wa Mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya sita (6) za Chamwino, Longido, Maswa, Mbinga, Mufindi na Songwe imefikia 90%.

64. Mhe. Spika, katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi itapima mipaka ya vijiji 200, kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi na mipangokina ya vijiji 200; itaandaa na kuidhinisha Hati za Hakimiliki za Kimila 200,000; kukarabati ofisi za ardhi za Halmashauri 41. Aidha, makazi 500,000 yatarasimishwa katika Halmashauri 23, Vituo 22 vya alama za upimaji vitaanza kujengwa na alama 276 za upimaji zitasimikwa. Vilevile, kumbukumbu za ardhi 1,647,330 zitabadilishwa kutoka analojia kwenda digitali; Mfumo Unganishi wa Kumbukumbu za ardhi (ILMIS) utasimikwa katika Halmashauri 132 na kujenga kumbi za mihadhara nne (4) katika Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro.

**Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu wa Upimaji ya Ramani (Land Data Infrastructure- Ldi).**

65. Mhe. Spika, katika mwaka 2022/23, Serikali iliahidi kuanza utekelezaji wa mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani wenye thamani ya dola za kimarekani milioni 65. Lengo la mradi huu ni kuweka miundombinu ya upimaji na ramani ambayo ita- ongeza kasi ya upangaji, upimaji ardhi na uandaaji wa ramani kwa matumizi mbalimbali. Utekelezaji wa mradi utaanza rasmi katika mwaka 2023/24.

Sambamba na mradi wa LDI, Wizara imeanzisha kituo kitakacho tumika kuwajengea watumishi uwezo, maarifa, ubunifu na matumizi ya teknolojia mpya ya mifumo ya kumbukumbu za ardhi, na menejimenti ya taarifa za kijiografia kwa ujumla.

**Ushiriki wa Wizara Katika Miradi ya Kimkakati**

66. Mhe. Spika, Katika kutekeleza Ibara ya 74(a) ya Ilani CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, Wizara kupitia Tume imeendelea kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwenye maeneo ya miradi ya Kimkakati. Kwa mwaka 2022/23, Tume ilipanga kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 75 katika maeneo yenye Miradi ya Kimkakati. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, jumla ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji 75 katika Halmashauri za Wilaya sita (6) za Kilosa (13), Rufiji (20), Mkalama (4), Kondoa (6), Bahi (10) na Ngorongoro (22) imeandaliwa. Aidha, katika mwaka 2023/24, Tume itaendelea kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi katika maeneo yenye Miradi ya Kimkakati.

**TAASISI NA BODI ZILIZO CHINI YA WIZARA Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)**

67. Mhe. Spika, katika mwaka 2022/23, Shirika lilipanga kukamilisha miradi ya Morocco Square, Kawe 711, Golden Premium Residence na PLOT 300 Regent Es- tate iliyopo Jijini Dar es Salaam iliyokuwa imesimama tangu mwaka 2018 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukosefu wa fedha.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan iliruhusu Shirika kukopa shilingi bilioni 173.9 ambapo hadi sasa Shirika limekopa shilingi bilioni 44.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo kama ilivyoelekezwa katika Ibara ya 75(i) ya Ilani ya CCM.

Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, mradi wa Morocco Square umekamilika kwa asilimia 100; Miradi ya Kawe 711 na Golden Premium Residence mazungumzo kati ya Shirika na wakandarasi yanaendelea ili kazi iweze kuen- delea na Mradi wa PLOT 300 Regent Estate hauku- tekelezwa kutokana na fedha iliyokuwa imetengwa ku- hamishiwa katika mradi wa nyumba za gharama nafuu wa Samia Housing Scheme uliopo Kawe.

68. Mhe. Spika, pamoja na ukamilishaji wa miradi ili- yokuwa imesimama kwa muda mrefu, Shirika pia liliahidi kukamilisha ujenzi wa nyumba 101 katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino na nyumba 303 katika Jiji la Dodoma eneo la Iyumbu kwa ajili ya kupangisha na kuuza ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa nyumba 1,000 Jijini Dodoma. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa nyumba 100 na jengo la maduka katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino umekamilika na ujenzi wa nyumba 300 na majengo matatu (3) ya huduma za kijamii katika Jiji la Dodoma (Iyumbu) umekamilika.

69. Mhe. Spika, sambamba na utekelezaji wa miradi ya nyumba za gharama ya kati, Shirika lilibuni mradi wa nyumba 5000 za gharama nafuu wa Samia Housing Scheme zitakazojengwa kwa awamu katika mikoa mba- limbali nchini kwa gharama ya shilingi bilioni 466. Kwa kuanzia, Shirika lilianzisha ujenzi wa nyumba 560 Kawe Jijini Dar es Salaam. Aidha, utekelezaji umefikia asilimia 15 na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2023/2024.

70. Mhe. Spika, katika mwaka 2022/23, Shirika limeendelea na utekelezaji wa miradi ya ukandarasi ikiwemo ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara nane (8) Jijini Dodoma katika Mji wa Serikali Mtumba. Wizara zinazohusika ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Nishati; Madini; Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Mifugo na Uvuvi; Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Utamaduni Sanaa na Michezo na Mambo ya Ndani ya Nchi. Miradi hiyo imefikia wastani wa 60%. Aidha, ujenzi wa Jengo la Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unaendelea na umefikia 56% na upanuzi wa jengo la Kitengo cha Moyo cha Jakaya Kikwete (JKCI) umefikia wastani wa 67%.

71. Mhe. Spika, Shirika pia linatekeleza miradi minne (4) ya ukandarasi wa ujenzi wa Ofisi za Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) katika Mikoa ya Pwani, Dodoma, Simiyu na Songwe yenye thamani ya shilingi bilioni 2.8 ambayo imefikia wastani wa 95%.

Aidha, Shirika linatekeleza mradi wa Serikali wa ujenzi wa jengo la Kituo cha Biashara Tanzanite (Tanzanite Trade Center) katika mji wa Mirerani Wilaya ya Simanjiro Mkoa wa Manyara ambao utagharimu shilingi bilioni 5.49. Mradi huu ulianza kutekelezwa Mei, 2022 na umefikia 70%. Vilevile, Shirika linatekeleza mradi wa ujenzi wa jengo moja la wagonjwa wa nje (OPD) katika Hospitali ya Ligula mkoani Mtwara. Ujenzi huo ulianza mwezi Aprili, 2022 na utakamilika mwezi Juni, 2023 kwa gharama yashilingi bilioni 2.7.

72. Mhe. Spika, Shirika lilizindua sera yake ya ubia iliyoboreshwa, tarehe 16 Novemba, 2022. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, miradi 24 ya ubia yenye thamani ya Shilingi bilioni 340 imepitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika. Hatua inayoendelea ni uandaaji wa mikataba ya ubia, upitishwaji wa mikataba husika na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Utiaji saini wa mikataba hiyo unatarajiwa kushuhudiwa na Mhe. Rais.

73. Mhe. Spika, katika mwaka 2022/23, Shirika lilipan- ga kukusanya shilingi bilioni 268.03 kutokana na vyan- zo mbalimbali ikiwemo shilingi bilioni 97.5 za kodi ya pango na shilingi bilioni 170.53 kutoka katika vyanzo vingine. Pamoja na changamoto ya wadaiwa sugu na wanunuzi wa nyumba kutokamilisha malipo kwa wakati, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Shirika limekusanya jumla ya shilingi bilioni 190 sawa na asilimia 71 ya len- go la kukusanya bilioni 268.03.

Kati ya hizo, bilioni 103 ni makusanyo ya kodi ya pango na bilioni 87 ni mapato yanayotokana na mauzo ya nyumba na miradi ya ukandarasi. Natoa rai kwa wadai- wa wote kulipa madeni yao kwa wakati ili kuliwezes- ha Shirika kuendelea kutoa huduma bora kwa watan- zania wengine.

74. Mhe. Spika, Shirika limeendelea kuboresha nyumba zake kwa kuzifanyia ukarabati katika mikoa mbalimbali nchini. Katika mwaka 2022/23, Shirika lilitenga shilingi bilioni 8 kwa ajili ya ukarabati wa majengo 200 yenye nyumba 2,000 katika mikoa ya Kilimanjaro, Shinyanga, Arusha, Mwanza, Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam na Katavi. Hadi tarehe 15 Mei, 2023, shilingi bilioni 6 zimetumika kukarabati majengo 153 yenye nyumba 1,500. Mhe. Spika, katika mwaka 2023/24, Shirika limepanga kuendelea na utekelezaji wa miradi mbali mbali mbali kama ilivyotajwa katika uk. 78 wa kitabu cha hotuba.

Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUPC)

75. Mhe. Spika, katika kutekeleza Ibara ya 74(b) ya Ilani ya CCM katika mwaka 2022/23, Wizara kupitia Tume ilipanga kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya nne (4) na vijiji 200 katika Halmashauri mbalimbali nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, Wizara kupitia Tume imewezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Halmashauri za Wilaya tatu (3) za Nsimbo (Katavi), Ngorongoro (Arusha) na Kigoma (Kigoma).

Aidha, jumla ya mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 306 sawa na 153% ya lengo, imeandaliwa katika Halmashauri za Wilaya 31 nchini (Jedwali Na. 14). Mipango hii inafanya kuwa na jumla ya vijiji 2,860 vyenye mipango ya matumizi ya ardhi kati ya vijiji12,318 vilivyopo nchini.

76. Mhe. Spika, Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2023, maeneo yenye ukubwa wa hekta 231,321 yametengwa kwa ajili ya malisho, hekta 199,110 hifadhi za misitu, hekta 23,215 misitu ya uvunaji, hekta 61,135 makazi, hekta 199,591 Kilimo na Mkazi, hekta 312,842 Kilimo, hekta 49,059 Uwekezaji, hekta 7,681 Huduma za Jamii, hekta 7,569 miundombinu, hekta 72,574 hifadhi ya vyanzo vya maji, hekta 11,378 ardhi ya jumla, hekta 2,572 ardhi ya akiba na matumizi mengine ni hekta 152,582 (Jedwali Na.15).

77. Mhe. Spika, katika mwaka 2023/24, Wizara kupitia Tume itaendelea kuandaa, kuwezesha, kuratibu na kusimamia mipango ya matumizi ya Ardhi ya Wilaya tano (5) na vijiji 410 ambapo mipango ya Wilaya tano (5) na vijiji 210 itaandaliwa kupitia fedha za ndani za maendeleo na mipango ya vijiji 200 itaandaliwa kupitia Mradi wa Uboreshaji Usalama wa Milki za Ardhi (LTIP). Pamoja na jitihada za Wizara kupitia Tume katika utekelezaji wa jukumu hili natoa Rai kwa Halmashauri za Wilaya zote nchini kutoa kipaumbele katika kutenga Fedha za uandaaji na utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Aidha, uandaaji wa mipangokina ya vitovu vya vijiji na mashamba, uwezeshashaji wa mamlaka za upangaji na uhuishaji wa mipaka ya vijiji na kazi nyingine za Tume umefafanuliwa katika uk. 83 – 87 wa kitabu cha hotuba.

Vyuo vya Ardhi na Bodi za Wataalam wa Fani za Ardhi

78. Mhe. Spika, Wizara pamoja na majukumu mengine ina jukumu la kusimamia taasisi zilizo chini ya Wizara zikiwemo Vyuo vya Ardhi Morogoro na Tabora, Bodi mbalimbali za Wataalam wa Sekta ya Ardhi. Bodi hizo ni Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Usajili wa Wathamini na Baraza la Taifa la Wapima Ardhi. Majukumu ya Bodi hizi yanajumuisha kusajili wataalam wa sekta na kampuni za kitaalam, kusimamia weledi na maadili ya kitaaluma. (Utekelezaji wa majuku- mu wa Vyuo na Bodi hizi rejea Uk. 91 – 93).

**SHUKRANI**

79. Mhe. Spika, napenda pia kwa umuhimu wa pekee kutambua mchango wa viongozi wenzangu katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Ninamshukuru Naibu Waziri, Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb.), kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Mhandisi Anthony Damian Sanga, Naibu Katibu Mkuu Bi. Lucy Dominico Kabyemela, Kamishna wa Ardhi Bw. Nathaniel M. Nhonge, Wakurugenzi na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

80. Mhe. Spika, vilevile, napenda kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Ardhi wanaojumuisha Mamlaka za Serikali za Mitaa, sekta binafsi, Bodi za Kitaaluma, Kamati za Ugawaji Ardhi, washirika wa maendeleo wakiwemo Benki ya Dunia, Benki ya EXIM ya Korea Kusini, UN-HABITAT, Shelter Afrique, African Union Comission, Benki ya Maendeleo Afrika, taasisi za fedha za ndani, Asasi za kiraia, mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu ya kisekta.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2023/24**

81. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu 48) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) kama ifuatavyo: - Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

| | | |
|---|---|---|
| | MAPATO | SHILINGI |
| A | Mapato ya Serikali | 300,000,000,000.00 |
| | MATUMIZI | |
| B | Matumizi ya Kawaida: | |
| | Mishahara (PE) | 43,428,651,000.00 |
| | Matumizi Mengineyo | 37,614,584,000.00 |
| | Jumla Ndogo | 81,043,235,000.00 |
| C | Matumizi ya Maendeleo: | |
| | Fedha za Ndani | 14,006,000,000.00 |
| | Fedha za Nje | 68,120,645,000.00 |
| | Jumla Ndogo | 82,126,645,000.00 |
| | **JUMLA MATUMIZI** | **163,169,880,000.00** |

Jumla ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Fungu48 ni shilingi 163,169,880,000.

Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu 03) Sura ya Bajeti ya Tume kwa mwaka 2023/24

82. Mhe. Spika, katika mwaka 2023/24, Tume inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 8.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Maendeleo kama inavyoonekana hapa chini: -

Fungu 03: Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

| AINA | AINA YA MATUMIZI | SHILINGI |
|---|---|---|
| A | Mapato | |
| | Mapato ya Serikali | 18,000,000 |
| B | Matumizi ya Kawaida; | |
| | Mishahara (PE) | 2,498,904,000 |
| | Matumizi Mengineyo | 2,293,724,000 |
| | Jumla Ndogo | 4,792,628,000 |
| C | Matumizi ya Maendeleo | |
| | Fedha za ndani | 3,410,000,000 |
| | Jumla Ndogo 3,410,000,000 | |
| **JUMLA KUU (B+C)** | | **8,202,628,000** |

83. Mhe. Spika, jumla kuu ya fedha zinazoombwa na Wizara (Fungu 48 na Fungu 03) ili Bunge liweze kuja- dili na kuidhinisha ni shilingi 171,372,508,000.00.

84. Mhe. Spika, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ambayo ni http://www.lands.go.tz.

85. Mhe. Spika, nakushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Ninaomba ku- toa hoja.





Mbunge Viti Maalumu, Halima Mdee akichangia hotuba ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi mwaka wa fedha wa 2023/2024, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vijana 45,000 kunufaika na mradi wa ujasiriamali

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi amezindua mradi wa USAID Kijana Nahodha unaolenga kuwafikia vijana 45,000 watakaonufaika na masuala ya elimu ya uongozi, ujasiriamali, afya na ujuzi.

Akizungumza jana kwenye uzinduzi wa mradi huo unaotekelezwa na Shirika la T-MARC Tanzania kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Watu wa Marekani (USAID), Katambi alisema mradi huo ni muhimu katika kuwezesha maendeleo ya kiuchumi hasa katika kuwajengea vijana uwezo wa kutumia vizuri rasilimali zilizopo ili kuleta maendeleo katika jamii.

"Aidha, miradi ya aina hii ni uthibitisho wa ushirikiano thabiti na dhati uliopo baina ya Tanzania na Marekani, tunatambua mradi huu wa kijana nahodha utasaidia kufikia malengo tuliyokusudia ya kumkwamua kijana wa kitanzania azione fursa na kuwa na mchango kwa Taifa lake,"alisema.

Naibu Waziri Katambi aliwataka vijana wa mikoa ya Dar es salaam, Morogoro na mikoa yote ya Zanzibar kuchangamkia fursa ya mradi huo.

"Niwaombe pia viongozi na maofisa mliopo wa wizara zote zinazohusika na utekelezaji wa mradi huu kutoa ushirikiano ili kuhakikisha mradi huu unatekelezwa ipasavyo kwa kuzingatia sera na miongozo ya nchi iliyopo ili kuweza kuleta tija kwa maslahi mapana ya taifa letu kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya vijana nchini,"alisema.

Naye, Mkurugenzi Mkazi wa USAID, Kate Somvongsiri, alipongeza serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa jitihada za kuwainua vijana.

"Mradi huu utaleta manufaa kwa Tanzania na ni muhimu vijana wakatumia fursa ya mradi huu, nchi inayowekeza kwa vijana inapiga hatua kimaendeleo,"alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la T-MARC Tanzania, Charles Singili, alisema mradi utainua vijana kufikia ndoto zao na unatekelezwa kwa kuzingatia sheria, taratibu na miongozo ya nchi.

Mkurugenzi wa mradi huo, Dk.Tuhuma Tulli, alisema utatekelezwa kwa miaka minne (2022-2026) na unalenga kusaidia vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 25 hususan vijana ambao hawana elimu ya shuleni, wasio na ajira, wenye ulemavu, wasichana waliozaa katika umri mdogo na wenye maambukizi ya VVU.

Alisema mradi huo unafadhiliwa na USAID kwa Dola za Marekani Milioni 10.6 na utaenda kuboresha upatikanaji wa elimu ikiwa ni pamoja na elimu ya ufundi stadi, afya, uraia, ujasiriamali na uongozi.

# Wakulima wahimizwa kutumia mbegu bora za mazao

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKAGUZI wa mbegu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Evatha Yamah amewataka wakulima kutumia mbegu bora za mazao zilizothibitishwa na wataalamu wa kilimo ili kuendesha kilimo chenye tija ikiwamo kupata mavuno mengi.

Alibainisha hayo alipotembelea wakulima wa halmashauri hiyo kwenye siku ya shamba la mkulima iliyoandaliwa na Shirika la Uzalishaji Mbegu za Kilimo Dodoma (DASPA) ili kuona namna wanavyoendesha kilimo chao.

Alisema ili mkulima avune mazao mengi msimu wa kilimo unapaswa kutumia mbegu bora ambazo zimethibitishwa ubora na wataalamu wa kilimo hivyo ni vema kuzingatia maelekezo wanayopewa na wataalamu.

Aliwataka wakulima kutumia fursa ya kulima mtama ili kujiinua kiuchumi kutokana na zao hilo kustawi kwa wingi mkoani Dodoma.

Katibu Mtendaji wa DASPA, Aithan Chaula aliwataka wakulima kutumia fursa ya kilimo cha karanga kwa kutumia mbegu bora ili isambae kwa wakulima wengine jambo litakalosaidia kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

Alisema kilimo cha karanga ni muhimu sana hivyo wakulima wanapaswa kulima na kuongeza uzalishaji wa mbegu hizo.

Makamu Mwenyekiti wa DASPA, Janeth Wilson alisema katika kuadhimisha siku ya shamba la mkulima, wakulima wamekuwa wakikimbushwa kutumia mbegu bora na kuendeleza kilimo cha mtama aina ya mesia na karanga.

Alisema wamekuwa wakisisitiza wakulima kulima mtama aina ya mesia ambayo inastahimili ukame pamoja na kukomaa kwa muda mfupi pindi unapopandwa shambani.

Alisema: "Wakulima wa Dodoma walime mtama unastawi vizuri, waachane na kilimo cha mazoea cha mahindi ambayo hayastawi sana katika baadhi ya maeneo kutokana na kuwa na mvua chache".

# Wananchi mikoa saba kunufaika na mradi ufugaji kuku

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MRADI wa kuboresha mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki (BEVAC) umepanga kuwafikia wananchi 10,000 katika mikoa saba.

Lengo la mradi huo ni kuongeza kiwango cha uzalishaji asali na Tanzania ifikie asilimia 20 ya uuzaji wa bidhaa hiyo katika soko la nje.

Meneja wa mradi huo unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na kutekelezwa na Shirika la Maendeleo la Ubeligij, Martin Mgallah, akizungumza na Nipashe jana, alisema tangu mradi huo umeanza mwaka 2021 umeshawafikia wafugaji nyuki zaidi ya 3,000.

Alisema mahitaji ya asali ya Tanzania katika soko la nje katika ni makubwa lakini kiwango kinachosambazwa ni asilimia nne tu ambacho kimekuwa kikiuzwa katika nchi za Ulaya, Marekani na Urabuni na hivi sasa limepatikana soko jipya la asali nchi Poland.

Mgallah alisema siyo kwamba Tanzania haina uwezo wa kuzalisha asali ya kutosha bali tatizo asali nyingi inapotea kwa sababu ya kukosa ubora.

"Masoko ya nje yana viwango vinavyotakiwa hivyo kinachofanywa na BEVAC ni kuwafundisha wafugaji nyuki ili asali nyingi isipotee iweze kuingia kwenye soko kubwa ambalo lina tija na litaweza kuingizia nchi fedha za kigeni," alisema.

Mgallah alisema mradi huu ambao ni wa miaka minne ulianzishwa kutokana na serikali kuona sekta ya nyuki haina msukumo mkubwa wakati asali ina soko kubwa nje lakini asali ya Tanzania ilikuwa inakosa ubora kwasababu wafugaji walikuwa wakifuga nyuki kwa njia za kienyeji.

"Tanzania ni nchi ya pili Afrika kwa kuzalisha asali ya kwanza ni Ethiopia na asali ya Tanzania iliyobora inatoka katika misitu ambayo ni asili hivyo masoko ya Ulaya yanapenda sana asali ya Tanzania. Kuanzishwa kwa mradi wa BEVAC ilikuwa ndio suluhisho la kutatua changamoto ya asali," alisema.

Mgallah alisema BEVAC imekuwa ikiwaunganisha wazalishaji wa asali wa mikoa ya Singida, Kigoma, Shinyanga, Katavi, Tabora, Pemba Kusini na Pemba Kaskazini ambako mradi huo unatekelezwa na masoko ya ndani na nje kwa kuwawezesha ili kuyafikia masoko hayo. Alisema: "Wafugaji wa nyuki walijenga fikra kwamba mizinga ni bidhaa ya kupewa lakini sasa hivi elimu tunayowapa tunataka waachane na kutumia mizinga ya kienyeji ambayo kwanza inasababishwa uharibifu wa mazingira tunataka watumie mizinga ya kisasa ambayo hata uzalishaji wa asali ni mkubwa".





Kaimu Mkurugenzi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA) Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Erast Saronga (kulia) akitiliana saini mkataba wa ujenzi wa mradi wa maji na Mkurugenzi wa Mtendaji wa Kampuni ya Jamta Construction Investment, Dk. Albert Katagira (katikati), utakaojengwa kwa muda wa miezi 15 katika kata ya Chimala, wilayani Mbeya na kampuni mbili, katika hafla iliyoshuhudiwa na Mkuu wa Mkoa Mbeya, Juma Homera (hayupo pichani), Ofisini kwake jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Vumwe Construction Investment, Mhandisi Kundaeli Mfwangavo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Madereva malori ya mchanga waandamana kisa tozo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MADEREVA wa malori ya mchanga jijini Mbeya, wameandamana hadi Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, kuiomba serikali iingilie kati mgogoro uliopo baina yao na viongozi wa umoja wao wakiwatuhumu viongozi wao kutumia vibaya fedha za tozo walizojiwekea.

Madereva hao waliandamana jana kutoka eneo la Ilomba zilipo ofisi zao hadi Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya kumuomba aingilie kati suala lao kuhusu matumizi mabaya ya fedha kwa viongozi wao.

Miongoni mwa madereva hao, Innocent Mlaye alisema kuwa wamechoshwa na mrundikano tozo za ushuru ikiwamo madini na ya umoja wa madereva ambayo alidai wameelekezwa kutoa zote katika risiti moja.

Hata hivyo alitilia shaka kwamba risiti ya ushuru hoo hauna maelekezo ya kiasi gani kinachokatwa kwenda kodi ya Ongezeko la Thamani VAT na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji EWURA.

Iman Mwampondele alisema wanashangazwa na ongezeko la ushuru wa madini kutoka Sh.3,000 hadi Sh.6,000 na kwamba imepanda bila ya wao madereva kushirikishwa kuhusu ongezeko hilo.

"Tunaiomba serikali iturudishie tozo ya Sh. 3,000 ya awali badala ya Sh. 6,000 ambayo imewekwa na viongozi wao bila ya sisi kushirikishwa, tumeamua kumwendea Mkuu wa Wilaya ili kuingilia kati suala hili yawezekana ni njama za viongozi wetu kujipatia kipato kipitia ushuru huu ambao hawatoi ufafanuzi kwa ongezeko," alisema Mwampondele.

Baada ya kusikiliza kero za madereva hao, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa aliagiza umoja huo wa madereva kuandaa mkutano mkuu ndani ya siku tatu ambao utamfanya achukue uamuzi wa kufuta umoja huo au kuacha uendelee. Alisema kama tozo hiyo haina msaada kwa wanachama ni vyema ikaondolewa na kwamba mkutano mkuu wa dharura utaamua nini cha kufanya.

Alisema: "Kitu ambao hakina faida ni ngumu kuwaambia watu waendelee kukitoa, sasa ili kufikia muafaka nimekaa na viongozi wenu kumaliza suala hilo ndani ya siku tatu kabla ya kuuvunja umoja huo ambao hauwanufaishi wananchi".

# 38% wanaoishi na VVU wabainika na shinikizo la damu

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

ASILIMIA 38 ya watu wenye maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) wamebainika kuwa na ugonjwa wa shinikizo la damu hali inayowaweka hatarini kupata magonjwa yasiyoambukiza.

Asilimia hiyo ni kati ya watu 722 waliofanyiwa utafiti na Kituo cha Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu nchini (NIMR) Kanda ya Mbeya ambapo kati yao 650 wamebainika kuwa na maambukizi na 122 hawana maambukizi.

Mtafiti Mkuu Mwenza wa Utafiti wa kundi la watu wa Afrika AFRICOS ambaye pia ni Mtafiti Mwandamizi wa NIMR Kanda ya Mbeya, Dk. Lucas Maganga alitoa taarifa hiyo jana wakati akizungumza na watumishi kutoka ubalozi wa Marekani na Shirika la HJFMRI.

Taarifa ya Dk. Maganga ni sehemu ya utekelezaji wa afua mbalimbali za kupambana na UKIMWI katika kuadhimisha miaka 20 ya mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU kupitia mfuko wa dharura wa Rais wa Marekani wa kupambana na Ukimwi (PEPFAR) na washirika wake WRAIR-DOD na HJFMRI mkoani Mbeya.

Alifafanua kuwa katika jitihada za mapambano dhidi ya VVU, NIMR kupitia utafiti wa kundi la watu wa Afrika ambao unafanya kazi na nchi nne za Afrika ikiwamo Tanzania, Afrika Kusini, Nigeria na Kenya umesaidia kuboresha huduma za matibabu kama vile upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya ugonjwa huo.

"Tunaishukuru Marekani kwa kutuwezesha sisi NIMR kufanya utafiti katika kutekeleza afua mbalimbali za UKIMWI na kifua kikuu ambapo katika kituo chetu tunafanya kazi na Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya MZRH na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya," alieleza Dk. Maganga.

Mtafiti wa VVU na UKIMWI NIMR Kanda ya Mbeya na Mratibu wa AFRICOS, Dk. Reginald Gervas alisema kuwa utafiti huo ni wa kwanza kuwahusisha watu wa Afrika na kwamba utasaidia matibabu rafiki kwa wananchi.

Alisema awali utafiti kuhusu maambukizi ya VVU ulikuwa unafanyika nchi zilizoendelea hivyo utafiti huu kuhusisha waafrika itasaidia kutoa tiba sahihi kwa watu wanaoishi na ugonjwa huo.

"Utafiti wa AFRICOS ambao unasaidia utafiti wa UKIMWI umesaidia kuboresha sera ya matibabu, kupunguza usugu wa dawa, pamoja na kushauri wa upatikanani wa huduma za pamoja za UKIMWI na magonjwa yasiyoambukizwa,"alisema Dk. Gervas.

Meneja wa NIMR Nyanda za Juu Kusini, Dk. Nyanda Ntinginya alisema wameendelea kufanya utafiti na kuratibu utafiti wa AFRICOS pamoja na maabara inayotembea ili kuwapatia wananchi tiba sahihi ya maambukizi ya VVU.

Alisema PEPFAR iliisaidia serikali kuanzisha maabara ya kisasa ambayo imesheheni vipimo ili kufanya utafiti wenye kuleta majawabu ya tiba sahihi.

Alisema kuwa NIMR Mkoa wa Mbeya ilianza kufanya utafiti wake mwaka 2013 kwa ajili ya kupata takwimu sahihi za maambukizi ya VVU na magonjwa nyemelezi, masuala ya kibaolojia, usugu wa dawa na namna ya utoaji wa huduma za dawa.

Mshauri wa Kinga za UKIMWI wa Shirika la WRAIR-DOD ya ubalozi wa Marekani, Dk. Alick Kayange alisema wanajivunia kuona utekelezaji wa afua mbalimbali za UKIMWI unawanufaisha wananchi kupitia wadau mbalimbali ambao umesaidia upatikanaji wa huduma za matibabu maeneo yote nchini.

# RUWASA yasaini mkataba ujenzi mradi wa maji Chimala

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA), Mkoa wa Mbeya, umesaini kandarasi ya ujenzi wa mradi wa maji katika Kata ya Chimala Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya na kampuni mbili ambazo zitatekeleza kwa miezi 15.

Kaimu Meneja wa RUWASA, Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Erast Saronga jana alisaini kandarasi hiyo katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya na kampuni ya Jamta Construction Investment Limited ya jijini Dar es Saalam na Vumwe General Services and Supplies Limited.

Alisema hadi kukamilika kwa mradi huo Sh. bilioni 4.5 zitatumika na kwamba utahusisha ujenzi wa banio la kutekea maji la ujazo wa lita 64.5, ujenzi wa tangi la ujazo wa lita 1,000 pamoja na ununuzi na ulazaji wa mabomba yenye urefu wa kilomita 60.

"Ujenzi huu utagharimu Sh. bilioni 4.5 hadi kukamilika kwake katika kipindi cha miezi 15 na kwamba utakuwa na manufaa makubwa kwani kitasimamiwa na chombo cha watumiaji maji CBWSO katika maeneo yao," alisema.

Akizungumza wakati wa kusaini mkataba huo wa ujenzi, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema utakapokamilika utawahudumia wakazi 38,086 na kuongeza huduma ya upatikanaji wa maji kutoka asilimia 54.8 hadi 62.6 wilayani Mbarali lakini pia kwa Mkoa wa Mbeya kutoka asilimia 64 hadi 66.

Aidha aliwataka makandarasi kujenga miradi hiyo kwa kuzingatia ubora unaotakiwa sambamba na kuzingatia muda wa kukamilisha mradi huo ili wananchi waanze kupata huduma ya maji hasa maeneo ya kutolea huduma za kijamii ikiwamo hospitali.

Mkandarasi anayetekeleza mradi huo kutoka Kampuni ya Vumwe Construction Investment, Kundaeli Mfwangavo aliomba serikali kupunguza baadhi ya tozo kwa makandarasi kwa madai kuwa wanafanya kazi ya kujenga miradi ya maendeleo kuwasaidia wananchi.

Dk. Albert Katagira wa Kampuni ya Ujenzi ya Jamta Construction Investment Limited aliiomba serikali kukamilisha malipo yao kwa wakati.

# Dk. Mwinyi ahimiza kulinda, kuhifadhi Bahari ya Hindi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema vipaumbele vya maendeleo ya Tanzania vinafungamana na Bahari ya Hindi hivyo ni vyema kuilinda na kuihifadhi bahari hiyo.

Aliyasema hayo wakati akifungua mkutano wa tisa wa mazungumzo ya Bahari ya Hindi uliofanyika visiwani Zanzibar, ambapo hotuba yake ilisomwa na Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman kwa niaba yake.

Alisema mabadiliko ya haraka ya kiuchumi yameathiriwa kwa kiasi kikubwa na mfumo ikolojia wa biashara ya baharini wa huduma za baharini, biashara na miundombinu ya bandari. "Tumebarikiwa, hakika tumepewa zawadi ya Zanzibar kama paradiso ya utalii katika ukanda huu. Tunaendelea vyema katika kugusa na kutumia kwa uwajibikaji gesi asilia ya nje ya nchi na vyanzo vingine vya nishati,"alisema.

Dk. Mwinyi alisema Tanzania ni taifa linalochipukia katika adhma ya uvuvi wa bahari kuu na wakati huo huo kubadilisha maisha ya wavuvi na jamii za wafugaji wa samaki.

Aidha, alisema kuna haja ya kuimarisha uwezo na kuendeleza mihimili ya ulinzi kuelekea ufadhili wa rangi ya buluu na hali ya hewa ambayo inanufaisha jamii. "Hii itakuwa ushindi kwa uchumi wa buluu, ustahimilivu wa bahari duniani, kukabiliana na hali ya hewa, usawa wa kijamii na malengo ya maendeleo endelevu"alisema.

Hata hivyo alisema uwezeshaji wa wanawake na ujumuishaji wa jinsia katika uchumi wa buluu ni muhimu ili kuleta ufanisi wa uchumi jumuishi, unaojumuisha na wenye ushirikiano.

Naye Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Masoud Suleiman Makame alisema, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua ungwaji mkono na ahadi za IORA, kuelekea kuinua matarajio ya uchumi wa buluu.

"Sote tunakubali kwamba ili uchumi wa buluu ufanikiwe, tunahitaji kuunganisha vipaumbele vyetu vya maendeleo na uendelevu, ushirikishwaji wa kijamii, na ushiriki wa sekta ya kibinafsi, katika ajenda yetu ya maendeleo ya bahari"alisema Waziri huyo.

Aidha, alisema kujitolea kwa viongozi wa nchi Rais Samia na Rais Dk. Mwinyi kuelekea mazungumzo ya kikanda na kimataifa kuhusu uchumi wa buluu na utawala wa bahari, kumerejesha nafasi ya Tanzania miongoni mwa familia za mataifa, kwa kufuata diplomasia ya uchumi wa pande zote kwa manufaa ya watu wake wote.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais wa Zanzibar Ikulu, Jamal Kassim Ali (kulia), akizungumza na Balozi Mdogo wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) anayefanyia kazi zake Zanzibar, Saleh Ahmed Al-Hemeiry (katikati), Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Watoto wachanga 1,567 wafariki dunia ndani ya miezi 8

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imekiri kuwapo kwa ongezeko la vifo vya watoto wachanga wakati na baada ya kujifungua ambapo kuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya vifo vya watoto wachanga 1,567 vimeripotiwa Unguja na Pemba.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri huyo, Hassan Khamis Hafidh katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Konde Zawadi, Amour Nassor aliyetaka kujua sababu za kuongezeka kwa vifo hivyo.

Alisema idadi hiyo ni kubwa ikilinganishwa kipindi kama hicho cha mwaka 2021/2022 ambapo vifo vilikua 1,201 kati ya 1,567 vilivyoripotiwa vifo 446 sawa na asilimia 28.5

Alisema miongoni mwa sasabu za kuongezeka kwa vifo hivyo ni kinamama wajawazito kuchelewa kwenda hospitali au vituo vya afya kwa ajili ya kujifungua.

Alisema wakati wanapofika katika vituo vya afya hospitali ni vigumu kufahamu matizo ambayo yanawakabili na wakati mwingine hupelekea kujifungua mlangoni au ndani ya gari.

Hafidh alisema pia upungufu mkubwa wa damu kwa mama wakati wa ujauzito ni miongoni mwa sababu ya ongezeko la vifo hivyo.

"Kutohudhuria kliniki kama ilivyoelekezwa na miongozo ya Wizara na miongozo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ambapo inaelekeza katika kipindi cha ujauzito mama anatakiwa kuhudhuria kliniki angalau mara nane kwa ajili ya kumfuatilia na kubaini kama kuna matatizo yoyote"alisema.

Alisema vifo hivyo vinaripotiwa karibu katika maeneo yote ya Zanzibar Mijini na vijijini lakini vinaripotiwa zaidi katika Kisiwa cha Unguja ukilinganisha na Pemba.

Aidha alisema licha ya jitihada zinazochukiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuajiri wafanyakazi bado kunaupungufu wa wafanyakazi hasa wauguzi na maofisa tabibu katika vituo vya afya vinavyotoa huduma za kuzalisha Unguja na Pemba.

"Katika jitihada za kupunguza vifo hivyo wizara inaendelea na jitihada za kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuhudhuria kliniki pamoja na kujifungua hopspitali,"alisema.

# 'Ukisababisha ajali Zanzibar unaadhibiwa hapo hapo'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imesema imeanza kutekeleza na kusimamia adhabu za hapo kwa hapo ambazo lengo lake ni kudhibiti ajali zinazosababishwa na uzembe kwa madereva wanaokiuka sheria za barabarani.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa wizara hiyo, Dk.Khalid Salum Mohamed wakati akiwasilisha makadirio mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023-2024 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Dk.Mohamed alisema wizara imechukuwa hatua hizo baada ya kubainika kujitokeza kwa ajali nyingi za barabarani ambazo kwa asilimia kubwa zinatokana na uzembe wa madereva.

Alisema ajali hiyo zimepoteza vifo vya wananchi wengi wa Zanzibar, njia pekee ambayo imeona ichukuliwe katika kukabiliana na majanga hayo ni adhabu za papo kwa papo.

Alisema utaratibu wa mchakato mzima wa kuanza kwa adhabu za papo kwa papo umekamilika ambao umewashirikisha wadau mbalimbali ikiwemo Jeshi la Polisi ambao watakuwa sehemu ya wasimamizi wa adhabu hizo.

Aidha alisema katika utafiti uliofanywa katika kipindi kifupi imebainika kwamba makosa yameanza kupungua ikiwemo yale yanayohusisna na uzembe.

Alisema katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Machi hadi April Sh.milioni 106 zimekusanywa na kuingia katika mfuko wa serikali.

Alisema Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imetoa leseni kwa madereva wa boda boda kwa lengo la kuwawezesha kujiajiri katika sekta binafsi.

Hata hivyo alisema kumejitokeza kwa matukio yanayokwenda kinyume na malengo ya kuanzishwa kwa biashara ya bodaboda ikiwemo vijana kujihusisha na matukio ya uhalifu na vitendo vya utovu wa nidhamu.

Alisema kuanzia Machi 2023 hadi Aprili makosa ya barabarani 4,910 yameripotiwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA, KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI NA. 25/2023**
**HAPPY GRATION ..............MWOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **IRENE EUSTACE**
- **JULIUS KAJUNA ....................WAJIBU MAOMBI**

**KWA: JULIUS KAJUNA (POPOTE PALE ULIPO)**
Unaarifiwa kuwa Maombi Na. 25/2023 yamepangwa kutajwa tarehe 03/07/2023 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, P.J. Makwandi saa 2:00 asubuhi.
HIvyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe / mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 16/05/2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**
**CIVIL CASE NO. 15 OF 2021**
**INNOCENT MALAMSHA............PLAINTIFF**
**VERSUS**
**SARAH MAKILULI...................1st DEFENDANT**
**MARY ANSELIM......................2nd DEFENDANT**
**ROMBO DISTRICT COUNCIL ............... 3rd DEFENDANT**
**SITEYA MELUBO MOLLEL ............... 4th DEFENDANT**
**THE HON. ATTORNEY GENERAL ......... 5th DEFENDANT**

**TO: 1. SARAH MAKILULI**
**2.MARY ANSELIM**

**NOTICE FOR MENTION**
**TAKE NOTICE:** That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 3rd day of July, 2023 at 09:00 am before Honorable Judge A.P. KILIMI.
**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT:** In default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.
**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this 15th day of May, 2023.

**Ag Deputy Registrar**
**Moshi**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.**
**Kituo cha NYABUBINZA mkoa wa SIMIYU**
**Shauri la Madai Na.04/2023**
**Jins la Mdai PAUL MAYUNGA BUDEDE**
**Jina la Mdaiwa 1.SHILINDE BUKOYE**
**2.NGUNYIWA NKUBA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA.**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa SHILINDE BUKOYE**
**KITONGOJI CHA SHISHIYU**
**K.K: VEO-SHISHIYU**
**MASWA.**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba(Eleza hapa habari za Madai)**
**MADAI YA FIDIA NA GHARAMA YA KUUZIWA ENEO MALI YA MTU MWINGINE KITAPELI KIASI CHA SHILINGI 2,500,000/- TU** Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 07 Mwezi 06 Mwaka 2023 saa 2;30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini .Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii Imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 24 Mwezi 05 Mwaka 2023

MAHAKAMA YA MWANZO NYABUBINZA MASWA
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO NYABUBINZA

---

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 51 OF 2023**

**In Matter of the Estate of the Late**
**ANTONY ELIA MASKATI**

**By 1. MARIA GASTON HATANGIMANA**
**2. ..................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the **05TH/06 / 2023.**
Dated at **Morogoro**, this **22** day of **05, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE DISTRICT COURT

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**VITUS KANISIUS KAPINGA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA PIAGGIO YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 683 CED.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/143768/2023**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 13/2023**
**In the Matter of the Estate of the Late**
**PHURAIM MBAZI MBWAMBO**
**And**
**In the Matter of the Application for Later of Administration BY HALIMA KATANA MAGOHE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grand of letters of Administration is made to the above names petitioner.
Objections to the grant should be filled on or before the 16 day of June, 2023.
Dated at Korogwe this 23 day of May, 2023.

DISTRICT COURT KOROGWE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE DISTRICT

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU VERONICA GIDION LYIMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T179ALT aina ya TOYOTA RAV4 Rangi ya KIJANI yenye Chasis No. 5XA11003507 Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **DOD/DOD/RB/149734/2023**

---

NJOO UTANGAZE
BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Uza, Chenye Thamani
Kubwa Kwa Kutangaza
Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ron DeSantis ajitosa mbio za urais Marekani

**NEWYORK,** MAREKANI

GAVANA wa Florida Ron DeSantis ametangaza rasmi nia yake ya kugombea katika kinyang'anyiro cha urais wa Marekani kwa mwaka 2024 kupitia tiketi ya Republican.

Gavana huyo aliyabainisha hayo jana kupitia mahojiano ya mtandao wa Twitter yaliyoongozwa na mmiliki wa jukwaa hilo la kijamii Elon Musk, ambayo yalilenga kutumika kama uzinduzi rasmi wa kampeni za DeSantis.

"Hakuna mbadala wa ushindi, lazima tukomeshe utamaduni wa kushindwa ambao umeambukiza chama cha Republican katika miaka ya karibuni, lazima tuangalie mbele, sio nyuma, tunahitaji ujasiri wa kuongoza na lazima tuwe na nguvu ya kushinda," alisema.

Kujitosa kwa DeSantis katika kinyang'anyiro cha tiketi ya Republican kunaweka mpambano mkali dhidi ya aliyewahi kuwa mshirika wake, Rais wa zamani Donald Trump, ambaye alishindwa katika uchaguzi wa rais wa 2020 na Mdemocrat Joe Biden.

Gavana huyo wa Florida anajinadi kama ofisa mkuu mtendaji aliyesimama kidete kuipinga serikali kuu kuhusu sera za UVIKO.

Alitetea sera zake jimboni Florida za kupiga marufuku ufundishaji wa dhana kama vile utambulisho wa kijinsia na ubaguzi wa kimfumo akisema ni njia ya kuwalinda watoto wadogo, pia katika siku za karibuni, alisaini hatua zinazozuia vikali utoaji mimba jimboni humo.

Huku wasifu wake ukiongozeka kitaifa na kile kinachotarajiwa kuwa rasilimali nyingi za kifedha, DeSantis (44), mara moja amekuwa mpinzani mkuu wa Trump kwa uteuzi wa tiketi ya Republican, na kwamba alionekana kumkosoa Trump isipokuwa hakumtaja moja kwa moja.

"Pia tunaelewa kuwa kuongoza serikali sio burudani, sio kujenga sifa yako au kutoa kauli za usahihi wa maadili, ni kuhusu kuleta matokeo, na matokeo yetu jimboni Florida yamekuwa bora zaidi," alisema.

Aidha, inaelezwa kuwa Trump, hakuchelewa kumkejeli DeSantis kwenye mtandao wake wa kijamii wa Truth Social, kutokana na mwanzo wa kuyumba wa kampeni yake.

"Uzinduzi wa DeSantis kwenye Twitter ni janga! Kampeni yake yote itakuwa janga," alisema.

Hata hivyo, jana DeSantis alijaza fomu katika tume ya uchaguzi ya Marekani, ikielezwa kuwa Gavana huyo anakabiliwa na kazi kubwa ya kuziba mwanya mkubwa wa umaarufu kati yake na Trump, huku Trump akiwa kifua mbele kwa karibu asilimia 40 ya pointi, licha ya kufunguliwa mashitaka ya uhalifu wa kifedha na kupatikana na hatia ya unyanyasaji wa kingono katika kesi ya mjini NewYork.

Wagombea wengine wa Republican waliotangaza nia yao ni pamoja na Nikki Haley, balozi wa zamani wa Marekani katika Umoja wa Mataifa, na Tim Scott, seneta wa Marekani kutoka South Carolina.

Mgombea mkuu wa Republican atakabiliana na Mdemocrat Joe Biden katika uchaguzi wa Novemba 2024.

**DW**

## Mfuasi wa Trump ahukumiwa kifungo gerezani

**WASHINGTON,** MAREKANI

MTU mmoja alietambulika kwa jina la Richard Barnett kutoka jimbo la

Arkansas nchini Marekani aliyepigwa picha akiwa ameweka miguu yake juu ya dawati, katika ofisi ya spika wa wakati huo wa Baraza la Wawakilishi la Marekani, Nancy Pelosi, amehukumiwa kifungo ch miaka minne na nusu gerezani.

Ilielezwa kuwa Barnett (63) alihukumiwa kifungo hicho jana, akidaiwa kujiunga na kundi la watu waliovamia majengo ya bunge la Marekani mwaka 2021.

Mfuasi huyo wa Trump, Barnett alipigwa picha na mpiga picha wa shirika la habari la AFP, akiwa amekalia kiti kwenye ofisi ya Pelosi, na picha hiyo ikawa mojawapo ya vielelezo vya uasi wa Januari 6, 2021 vilivyotumika kumtia hatiani.

Barnett alikuwa ameungana na wafuasi wa Rais wa wakati huo Donald Trump, ambao walivamia Bunge lilipokuwa likikutana kumuidhinisha Mdemokrat Joe Biden, kama rais ajaye wa Marekani.

Aidha, ilielezwa kuwa Mahakama hiyo ya mjini Washington, ilimtia hatiani Barnett mwezi Januari mwaka huu, kwa makosa manane, ikiwa ni pamoja na kuzuia bunge kuidhinisha uchaguzi, kuingia kinyume cha sheria katika majengo ya bunge na kusabaisha fujo na kutumia silaha hatari.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa waendesha mashtaka walikuwa wamemtaka Jaji Christopher Cooper kumhukumu kifungo cha miaka saba gerezani. **BBC**

**Ilielezwa kuwa Barnett (63) alihukumiwa kifungo hicho jana, akidaiwa kujiunga na kundi la watu waliovamia majengo ya bunge la Marekani mwaka 2021.**



Watoto wakimbizi wa Sudan ambao wamekimbia ghasia katika eneo laDarfur karibu na mpaka wa Sudan na Chad huko Koufroun. **PICHA: REUTERS.**

# Ukraine yasisitiza Afrika kuwa na msimamo

**KYIV,** UKRAINE

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Ukraine Dmytro Kuleba amezitaka nchi za Afrika kukomesha msimamo wao wa kutoegemea upande wowote kuhusu uvamizi wa Russia wakati akianza ziara ya pili barani humo.

Waziri huyo aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mji mkuu wa Ethiopia Addis Ababa.

"Kwa kutoegemea upande wowote dhidi ya uvamizi wa Russia dhidi ya Ukraine, unaonyesha kutoegemea upande wowote kwa ukiukaji wa mipaka na uhalifu mkubwa ambao unaweza kutokea karibu na wewe, ikiwa hautatokea kusaidia," alisema.

Pia Kuleba alibainisha kwamba uhusiano wa Ukraine na nchi za Afrika haukuzingatiwa ipasavyo katika sera yao ya mambo ya nje kwa miaka mingi na kwamba walipoteza mengi.

Aidha, ilielezwa kuwa kiongozi huyo alifanya mazungumzo na Waziri

Mkuu Abiy Ahmed, mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika Moussa Faki na Rais wa Comoro Azali Assoumani, ambaye ni mwenyekiti wa sasa wa Umoja wa Afrika (AU).

Hata hivyo, ilielezwa kuwa nchi sita za Afrika zikiongozwa na Afrika Kusini zinaongoza mpango wa amani kati ya Moscow na Kyiv kwani vita vinaathiri vibaya usambazaji wa nafaka na mbolea katika eneo hilo.

Wakati nchi nyingi zimekuwa zikilaani mara kwa mara uvamizi wa Russia wakati wa mijadala katika Umoja wa Mataifa (UN), kujiepusha kwa nchi mbalimbali za Afrika kumezua ukosoaji wa Magharibi.

Ziara ya Kuleba barani Afrika pia inajumuisha ziara za Morocco na Rwanda.

Alifanya safari yake ya kwanza barani humo Oktoba mwaka 2022 alipotembelea Senegal, Ivory Coast, Ghana na Kenya.

**BBC**

# MORRISON, GADIEL WATAJWA KUJIUNGA SINGIDA BIG STARS

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Singida Big Stars imeahidi kufanya usajili mkubwa na wenye tija kwa ajili ya kufanya vizuri katika msimu ujao ambao watashiriki mashindano ya kimataifa kwa kuwanasa, Bernard Morrison wa Yanga na Gadiel Michael anayeichezea Simba, imeelezwa.

**Hata hivyo tetesi zinasema klabu hiyo iko katika mchakato wa kumwachia kiungo mshambuliaji wake, Bruno Gomes ambaye anawindwa na Simba na Yanga.**

Ofisa Habari wa Singida Big Stars, Hussein Masanza, alisema jana wamejipanga kufanya usajili bora kwa sababu tayari wana uhakika wa kuiwakilisha Tanzania Bara katika michuano ya Kombe la Shirikisho na wanataka kufika mbali na si kusindikiza.




"Tuko katika mkakati mkubwa wa kuboresha kikosi chetu kwa sababu tayari tuna nafasi ya kucheza michuano ya kimataifa, Kombe la Shirikisho msimu ujao, tutakwenda kufanya usajili wa wachezaji bora wa ndani na nje ya nchi, sisi huwa hatukosei, wote wanajua, huwa tunaleta vifaa haswa," alisema Masanza.

Kuhusu mchezaji Bruno kuondoka katika klabu hiyo msimu huu, alisema haiwezekani wamwachie mchezaji bora kama huyo wakati wanakwenda kucheza mechi za kimataifa.

"Unakwenda kucheza mechi za kimataifa, halafu unamwacha Bruno? Hapana bado ataendelea kuwapo katika timu yetu kwa sababu na sisi tunataka kufanya vizuri siyo kusindikiza," Masanza alisema.

Alikataa kuthibitisha habari za kuwasajili wachezaji wataotajwa msimu ujao watatumikia kikosi hicho.

"Hao ni wachezaji wa timu nyingine, siwezi kuwazungumzia wachezaji wa klabu nyingine na usajili bado haujaanza, kila kitu kikiwa sawa tutawaeleza sisi wenyewe mchezaji yupi tumemsajili," alisema kiongozi huyo.

Singida Big Stars imepata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao kutokana na kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu, huku timu zilizoingia fainali katika Kombe la FA, Yanga na Azam, nazo tayari zina tiketi ya kucheza michuano ya kimataifa msimu ujao.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Dar es Salaam wakichuana kuwania mpira wakati wakifanya mazoezi ili kujiimarisha kwenye Uwanja wa Jakaya Kikwete jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Soka la ufukweni Zanzibar kesho

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

TIMU ya Pandani itakutana na Madaniwa katika mechi ya ufunguzi ya Ligi ya Ufukweni Zanzibar itakayochezwa kesho asubuhi wakati Wesha itawakaribisha Raha kwenye mchezo mwingine wa ligi hiyo.

Michezo yote itachezwa kwenye Ufukwe wa Vuma Wimbi ulioko Kisiwani Pemba.

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa Kamati ya Soka la Ufukweni wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), Sheha Mohamed Ali, alisema michuano hiyo itachezwa katika Kanda ya Unguja na Pemba.

Ali alisema kwa upande wa Kanda ya Unguja, mechi zitaanza kufanyika kuanzia mapema mwezi ujao na kuongeza jumla ya timu 10 zitashiriki katika Kanda ya Pemba na itakuwa ni ya Ligi Daraja la Kwanza.

Alisema timu nne zitakazofanya vizuri katika kila kanda zitatinga hatua ya nusu fainali na baadaye kucheza fainali ili kupata bingwa wa ligi hiyo katika msimu huu.

"Kwa mara ya kwanza tunaenda kucheza michuano ya soka la ufukweni kwa mfumo rasmi ambao upo kama ligi nyingine zinavyochezwa, zamani ilikuwepo soka la ufukweni ila kwa msimu huu tumeona tuboreshe zaidi ili kuendana na kasi ya soka lenyewe, " alisema Ali.

Aliongeza ZFF inazishukuru taasisi zote ambazo zimechangia ili kufanikisha ligi hiyo ikiwamo Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), ASAS, Azam, Ashton, Mamlaka ya Bandari Zanzibar na Wizara ya Michezo Zanzibar

## Odhiambo atajwa kutua Namungo FC

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Tanzania Prisons, Mkenya Patrick Odhiambo, anatajwa kurejea nchini ili kujiunga na kikosi cha Namungo FC kwa ajili ya maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu Bara.

Odhiambo anatajwa huenda akachukua nafasi ya Denis Kitambi ambaye ndiye kocha anayeifundisha timu hiyo ya mkoani Lindi kwa sasa.

Akizungumza na Nipashe jana, Odhiambo alisema suala la kuhusishwa na Namungo FC ni tetesi lakini aliweka wazi amepokea ofa mbalimbali kutoka katika timu za Tanzania.

Odhiambo alisema kwa sasa yuko katika mazungumzo na hizo timu na baada ya kuafikiana ataweka wazi ni klabu ipi ataifundisha.

Hata hivyo alisema hajafuatwa na mabosi wa Namungo FC yenye pointi 39 na iko katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, hivyo kwake anaziita ni tetesi.

## TADA kuchaguana Juni 25 Dodoma

**Na Shufaa Lyimo**

UCHAGUZI Mkuu wa Chama cha Mchezo wa Vishale Tanzania (TADA), umepangwa kufanyika ifikapo Juni 25, mwaka huu jijini Dodoma.

Ofisa wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Najaha Bakari, alisema fomu kwa ajili wanaotaka kuwania zimeshaanza kutolewa na usaili wa wagombea watakaokuwa wamejitokeza utafanyika Juni 24, mwaka huu jijini humo.

Alizitaja nafasi zinazowaniwa ni ya mwenyekiti, makamu mwenyekiti, Katibu Mkuu, Katibu Msaidizi, Katibu wa Mipango, Katibu Mwenezi na Mahusiano, Mweka Hazina, Mweka Hazina Msaidizi na Wajumbe wanne wa Kamati ya Utendaji ya chama hicho.

"BMT inatoa wito kwa yeyote mwenye sifa ya kugombea kwa mujibu wa katiba ya chama hiki (TADA), kujitokeza kuchukua fomu kwa ajili ya kukamilisha mchakato wa uchaguzi kwa maendeleo ya mchezo  wa vishale nchini," alisema Najaha.

Aliongeza BMT inasisitiza wanachama wa TADA wanatakiwa kuhakiki uhai wao kwa kulipa ada ili kupata sifa za kushiriki katika uchaguzi huo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### OSIMHEN KUIKAMUA UNITED

KLABU ya Manchester United haina budi kulipa pauni milioni 140 kama inataka kumsajili mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 24, msimu huu baada ya kuafikiana dili la mchezaji-mwenza na mlinzi wa Korea Kusini, Kim Min-jae mwenye miaka 26. (***Mirror***)

### NAPOLI YAMBANA KIM

NAPOLI wanajaribu kumshawishi beki wa Korea Kusini, Kim Min-jae, akubali kutia saini mkataba mpya kabla ya kifungu cha kuachiliwa kuanza kutumika msimu huu wa joto. (***90 Min***)

### ARTETA AMRUHUSU ROWE

MIKEL Arteta yuko tayari kumruhusu kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Emile Smith Rowe, mwenye miaka 22 kuondoka Emirates ili kutoa nafasi kwa kiungo wa Leicester, James Maddison (26). (***Mirror***)

### SANABRIA ATAJWA ARSENAL

ARSENAL wameonyesha nia ya kumwongeza mshambuliaji wa Torino na Timu ya Taifa ya Paraguay, Antonio Sanabria, mwenye umri wa miaka 26 kwa mkataba wa thamani ya pauni milioni 21. (***La Repubblica via Mail***)

### UNITED YAKOMAA NA KANE

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29, bado anasalia kuwa chaguo la kwanza la Manchester United na klabu hiyo inapania kuanza mapema kufanya mazungumzo na Spurs. (***Guardian***)

### REAL YAMTAKA ROCA

REAL Betis huenda ikafufua nia yao ya kumnunua kiungo wa kati wa Leeds United Mhispania, Marc Roca, mwenye umri wa miaka 26, ikiwa klabu hiyo ya Yorkshire itashushwa daraja kutoka Ligi ya Kuu England. (***Estadio Deportivo***)

### NELSON AGOMBEWA SOKONI

ARSENAL imempa kiungo wa England, Reiss Nelson, mkataba mpya hadi 2027, inayojumuisha chaguo la nyongeza ya mwaka, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 pia amepokea ofa kutoka kwa timu nyingine za Ligi Kuu England, Italia na Hispania. (***Fabrizio Romano***)

### MARTIN ATUA SOUTHAMPTON

KOCHA wa Swansea, Russell Martin, mwenye umri wa miaka 37 amekubali kutua katika kikosi cha Southampton. (***Sky Sports***)

### BARCA YAMSHANGAA KOUNDE

BARCELONA imeshangazwa na tetesi kuwa mlinzi wa Ufaransa, Jules Kounde, mwenye umri wa miaka 24 anataka kuondoka katika klabu hiyo, ikiwa ni mwaka mmoja tu baada ya kujiunga nao akitokea Sevilla. (***90 Min***)

### MOUNT AKARIBIA UNITED

KLABU ya Manchester United iko tayari kulipa pauni milioni 55 kumnunua kiungo wa Chelsea na England, Mason Mount, na nia yao kuzishinda Liverpool na Arsenal katika mbio za kuinasa saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. (***Mail***)

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# SOUTHGATE AAMUA KUMTEMA STERLING

**LONDON,** England

## ●●● Ni katika kikosi cha England kutokana na kusumbuliwa na...

RAHEEM Sterling ameachwa nje ya kikosi cha wachezaji 25 cha Timu ya Taifa ya England kitakachojiandaa na mechi za kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Euro 2024 zitakazochezwa mwezi ujao dhidi ya Malta na Macedonia Kaskazini huku Eberechi Eze na Lewis Dunk wakiitwa.

**Sterling amekuwa na wakati mgumu katika ubora na uti mamu wa mwili msimu huu baada ya kuhama kutoka Manchester City kwenda Chelsea kwa mkataba wa pauni milioni 47.5 msimu uliopita wa joto, akifunga mabao tisa na kutoa pasi nne za mabao katika mechi 37 alizocheza.**

Na baada ya kutaja kikosi chake jana, Kocha wa England, Gareth Southgate, alisema katika mkutano wa waandishi wa habari: "Nilizungumza naye wiki moja au zaidi iliyopita, tukio la kawaida. Hafurahii hali yake ya kimwili, amekuwa na tatizo la misuli ya paja.

"Kwa kweli hakuwa mtu wa furaha. Hafikirii kuwa anafanya kazi kwa kiwango anachohitaji kwa hiyo ndiyo mazungumzo niliyokuwa nayo naye."

Eze amefunga mabao sita katika mechi nane akiwa na Crystal Palace huku wakifufua bahati yao chini ya Roy Hodgson.

Bado hajacheza mechi yake ya kwanza ya wakubwa lakini alikosa kuwa sehemu ya kikosi cha muda cha England kwenye Euro 2020 baada ya kupata jeraha la kifundo cha mguu usiku wa kuamkia michuano hiyo.

"Tumempenda kwa muda mrefu," Southgate alisema kuhusu Eze.

"Alikuwa na bahati mbaya sana kabla ya michuano ya Euro. Tulikuwa tunaenda kumwita kwenye kambi ya maandalizi ili kumtazama na akapata jeraha baya.

"Nakumbuka nilizungumza na Roy Hodgson kuhusu yeye wakati huo na Roy aliniambia alikuwa amepata majeraha.

"Hivyo nadhani amemaliza msimu kwa nguvu sana, anaweza kucheza nafasi kadhaa kwenye safu ya ushambuliaji, ni tishio la goli, ana uwezo mzuri, kasi ya kupita watu na kuchukua watu. Tunatazamia kumwona karibu zaidi na kila mtu ninayezungumza naye anazungumza kwa ustadi kumhusu yeye."

Dunk aliitwa kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka minne na nusu baada ya kuimarika huko Brighton na kujiunga tena na kikosi cha England pamoja na Tyrone Mings wa Aston Villa, ambaye mechi yake ya mwisho ilicheza Machi 2022 dhidi ya Ivory Cost.

Kikosi kamili:

Makipa: Jordan Pickford, Aaron Ramsdale, Sam Johnstone.

Mabeki: Trent Alexander-Arnold, Lewis Dunk, Marc Guehi, Harry Maguire, Tyrone Mings, Luke Shaw, John Stones, Kieran Trippier, Kyle Walker.

Viungo: Jude Bellingham, Eberechi Eze, Conor Gallagher, Jordan Henderson, James Maddison, Kalvin Phillips, Declan Rice.

Washambuliaji: Phil Foden, Jack Grealish, Harry Kane, Marcus Rashford, Bukayo Saka na Callum Wilson.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,117,4
MECHI KALI
SAMPDORIA
VERSUS
SASSUOLO
1 | 3.55
X | 3.60
2 | 1.88
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LAMPARD: SISHANGAI MOUNT KUCHELEWA KUSAINI MKATABA



**LONDON,** England

FRANK Lampard amesema, Mason Mount, atasaini mkataba mpya na Chelsea "katika ulimwengu mzuri" lakini akakubali hali inaweza isiwe rahisi kwa kiungo huyo wa kati wa Timu ya Taifa ya England.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 anakaribia kuingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na amekuwa akihusishwa na kuhama katika klabu hiyo aliyojiunga akiwa na umri wa miaka sita.

Pande hizo zimekuwa katika mazungumzo kwa muda mrefu wa msimu huu kuhusu mkataba mpya lakini zimeshindwa kufikia makubaliano na inaonekana kuna uwezekano mkubwa ataondoka huku Liverpool na Manchester United wakiripotiwa kumtaka.

Ikiwa hakuna nyongeza iliyokubaliwa itamaanisha yuko huru kuanza kufanya mazungumzo na klabu nyingine mwanzoni mwa mwaka ujao, lakini Chelsea wanaweza kutafuta kumuuza msimu wa joto ili kuepusha uwezekano wa mhitimu huyo wa akademi kuondoka bure.

Lampard, ambaye alimpa nafasi ya kucheza kwa mara ya kwanza katika kikosi cha kwanza, Mount mwaka 2019 na mara kwa mara amekuwa akitoa pongezi kwake, alisema klabu lazima ifanye kazi kuwaonyesha wachezaji wa akademi kuna njia ya kuelekea upande wa wakubwa bila kujali mustakabali wa Mount.

"Ni jambo gumu kwangu kulizungumzia kwa sababu siko ndani ya kichwa cha Mason na kwa mtazamo wa klabu," alisema Lampard. Kwa maana ya vitendo ni kati ya pande zote mbili. Sishangai kwa sababu hili ni soka. Je! kila mtu anajua ninampenda sana Mason Mount kama mchezaji wa mpira? Ndiyo, hakika, bila shaka.

# Alba sasa kuondoka Barca



**BARCELONA,** Hispania

MAISHA ya Jordi Alba ndani ya Barcelona yatafikia tamati mwishoni mwa msimu huu baada ya wababe hao wa Ligi Kuu Hispania (LaLiga), kutangaza wamefikia makubaliano ya kusitisha mkataba wake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ambaye mkataba wake wa sasa ulipaswa kumalizika mwishoni mwa 2023/24, ameichezea klabu hiyo mara 458 na kushinda mataji 19 makubwa tangu alipocheza mechi yake ya kwanza dhidi ya Real Sociedad mwaka 2012.

Barcelona ilisema katika taarifa yake: "FC Barcelona inapenda kutoa shukrani zake hadharani kwa Alba kwa muda wake na kujitolea, na uhusiano wake mzuri na wa kirafiki na wanachama wote wa familia ya Barca, na inamtakia kila la kheri katika siku zijazo.

"Barca daima itakuwa nyumbani kwako, Jordi."

Alba alizaliwa Barcelona na alipitia timu ya vijana ya klabu kabla ya kuruhusiwa kuondoka mwaka 2005 kuelekea Valencia ambako alikua mchezaji wa kikosi cha kwanza kabla ya Barca kumrudisha Nou Camp mwaka 2012.

## HABARI MICHEZO

17,539/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/05/23 | 19:00 | ACF Fiorentina vs AS Roma | 2.40 | 3.20 | 2.75 |
| 02. 27/05/23 | 20:00 | Sevilla FC vs Real Madrid | 2.80 | 3.40 | 2.29 |
| 03. 27/05/23 | 22:00 | Montpellier HSC vs OGC Nice | 2.47 | 3.30 | 2.60 |
| 04. 28/05/23 | 02:30 | Orlando City SC vs Atlanta United FC | 2.15 | 3.10 | 2.85 |
| 05. 28/05/23 | 15:30 | Carlisle United vs Stockport County FC | 3.00 | 3.15 | 2.28 |
| 06. 28/05/23 | 15:30 | AZ Alkmaar vs PSV Eindhoven | 2.55 | 3.50 | 2.40 |
| 07. 28/05/23 | 15:30 | Fortuna Sittard vs NEC Nijmegen | 2.50 | 3.40 | 2.50 |
| 08. 28/05/23 | 16:00 | AC Monza vs US Lecce | 2.70 | 3.10 | 2.50 |
| 09. 28/05/23 | 17:15 | Racing Santander vs FC Cartagena | 2.55 | 3.05 | 2.65 |
| 10. 28/05/23 | 18:30 | Chelsea FC vs Newcastle United | 2.80 | 3.35 | 2.29 |
| 11. 28/05/23 | 18:30 | Aston Villa vs Brighton & Hove Albion | 2.16 | 3.55 | 2.90 |
| 12. 28/05/23 | 18:30 | Leeds United vs Tottenham Hotspur | 2.65 | 3.45 | 2.34 |
| 13. 28/05/23 | 20:00 | Cadiz CF vs RC Celta de Vigo | 2.65 | 3.15 | 2.50 |
| 14. 28/05/23 | 20:00 | Getafe CF vs CA Osasuna | 2.50 | 3.15 | 2.70 |
| 15. 28/05/23 | 20:00 | Girona FC vs Real Betis Seville | 2.60 | 3.15 | 2.60 |
| 16. 28/05/23 | 21:45 | Juventus Turin vs AC Milan | 2.26 | 3.25 | 2.95 |
| 17. 28/05/23 | 22:00 | SC Corinthians SP vs Fluminense FC RJ | 2.70 | 3.05 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 26/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 1981 | Legetafo Legedadi vs Adama City FC | 3.58 | 3.32 | 1.92 |
| 17:00 | 1952 | Bodrumspor vs Goeztepe | 1.94 | 3.29 | 3.44 |
| 18:00 | 3261 | Lahti vs AC Oulu | 3.02 | 3.17 | 2.16 |
| 18:00 | 3896 | Gomel vs Smorgon | 1.61 | 3.75 | 4.68 |
| 18:00 | 4399 | VPS Vaasa vs Ilves Tampere | 2.42 | 3.03 | 2.72 |
| 18:00 | 4721 | Saint George FC vs Bahir Dar Kenema FC | 2.10 | 2.85 | 3.20 |
| 19:00 | 1681 | OTP FC vs OLS Oulu | 3.83 | 3.62 | 1.78 |
| 19:00 | 4316 | Nea Salamis vs Olympiakos Nicosia | 1.65 | 4.00 | 4.43 |
| 19:00 | 5745 | Vsnk Varazdin vs Lokomotiva Zagreb | 2.54 | 3.33 | 2.40 |
| 19:30 | 4435 | Hobro vs HB Koge | 2.30 | 3.39 | 2.62 |
| 19:30 | 4552 | Fremad Amager vs Nykobing FC | 1.71 | 4.10 | 3.54 |
| 19:30 | 4769 | FC Fredericia vs Hillerod | 1.67 | 3.59 | 4.30 |
| 20:00 | 3602 | Sakaryaspor vs Eyupspor | 2.94 | 3.25 | 2.17 |
| 20:00 | 4164 | CD Feirense vs SCU Torreense | 2.39 | 3.18 | 2.76 |
| 20:00 | 4359 | Talaea El Gaish vs Al Ahly Cairo | 5.63 | 3.72 | 1.57 |
| 20:00 | 4670 | AFC Eskilstuna vs Gais | 3.99 | 3.62 | 1.84 |
| 20:00 | 4973 | Odense vs Horsens | 1.68 | 3.90 | 4.46 |
| 20:15 | 3448 | Floridsdorfer AC vs SKN St Polten | 2.95 | 3.31 | 2.18 |
| 21:00 | 4213 | Rio Ave vs Famalicao | 2.50 | 3.16 | 2.71 |
| 21:00 | 4712 | Almere City vs FC Eindhoven | 1.63 | 3.62 | 5.02 |
| 21:30 | 1545 | Zalaegerszegi TE vs Paksi FC | 2.55 | 3.16 | 2.55 |
| 21:30 | 2233 | Sudtirol vs Reggina | 2.37 | 2.94 | 3.04 |
| 21:45 | 1120 | Sampdoria vs Sassuolo | 3.55 | 3.60 | 1.88 |
| 21:45 | 1161 | Caen vs St Etienne | 2.44 | 3.40 | 2.60 |
| 21:45 | 1668 | Bohemians FC vs Shelbourne | 1.94 | 3.09 | 3.71 |
| 21:45 | 1932 | Laval vs Nimes | 1.50 | 4.00 | 5.80 |
| 21:45 | 2427 | Rodez Aveyron vs PAU FC | 2.20 | 3.25 | 3.05 |
| 21:45 | 2633 | US Quevilly Rouen vs Amiens | 2.36 | 3.30 | 2.75 |
| 21:45 | 3108 | St Patricks vs Dundalk FC | 1.84 | 3.45 | 3.60 |
| 21:45 | 3136 | Sochaux vs Metz | 3.76 | 3.56 | 1.84 |
| 21:45 | 3142 | Drogheda Utd vs UCD Dublin | 1.46 | 4.00 | 5.75 |
| 21:45 | 3189 | Valenciennes vs Grenoble Foot | 1.88 | 3.49 | 3.69 |
| 21:45 | 3303 | Guingamp vs Niort | 1.56 | 4.00 | 5.00 |
| 21:45 | 3944 | Annecy FC vs Bordeaux | 4.11 | 3.50 | 1.78 |
| 21:45 | 4803 | Bray Wanderers vs Cobh Ramblers | 1.75 | 3.65 | 3.80 |
| 21:45 | 5246 | Bastia vs Le Havre | 2.50 | 3.05 | 2.75 |
| 21:45 | 5389 | Dijon vs Paris FC | 1.83 | 3.51 | 3.86 |
| 21:45 | 5535 | Ayr United vs Partick Thisle | 2.23 | 3.42 | 2.90 |
| 21:45 | 5969 | Cork City vs Shamrock Rovers | 5.54 | 3.90 | 1.49 |
| 22:00 | 1575 | Sedan vs Villefranche Sur Saone | 2.69 | 3.32 | 2.43 |
| 22:00 | 1619 | Le Puy vs Bastia Borgo | 1.68 | 3.74 | 4.53 |
| 22:00 | 2474 | Orleans vs Concarneau | 3.62 | 3.41 | 1.94 |
| 22:00 | 3971 | Le Mans vs Dunkerque | 2.43 | 3.35 | 2.67 |
| 22:00 | 3974 | Paris 13 Atletico vs Chateauroux | 3.20 | 3.36 | 2.11 |
| 22:00 | 4083 | Bourg Peronnas vs Nancy | 2.36 | 3.37 | 2.74 |
| 22:00 | 4291 | Zaragoza vs Tenerife | 2.51 | 3.11 | 2.71 |
| 22:00 | 5358 | Avranches vs Cholet | 1.89 | 3.62 | 3.57 |
| 22:00 | 5400 | FC Martigues vs FC Versailles 78 | 1.82 | 3.46 | 4.04 |
| 22:00 | 5597 | Red Star vs Saint Brieuc | 1.53 | 4.16 | 5.27 |
| 23:15 | 3631 | FC Vizela vs Sporting Lisbon | 5.24 | 4.23 | 1.52 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# YANGA KAMILI KUIMALIZA USM ALGER KWA MKAPA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umesema tayari umekamilisha maandalizi kwa ajili ya mchezo wa kwanza wa fainali ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya USM Alger kutoka Algeria utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kikosi kinaendelea vizuri na mazoezi na wamejipanga kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ili kuimaliza mechi hiyo hapa nyumbani.

Kamwe alisema wakati benchi la ufundi likiendelea na majukumu yao, viongozi leo watakuwa na shangwe la fainali hizo kwenye viwanja vya Zakhiem, Mbagala, Dar es Salaam kwa ajili ya kuhamasisha mashabiki kujitokeza kwa wingi kushuhudia mchezo huo.

"Hii ni mara ya kwanza kucheza fainali, viongozi wako makini sana na kutuliza akili ili kufanikisha malengo yetu ya kushinda nyumbani na kupata matokeo ugenini ili Juni 4, mwaka huu turudi na Kombe la Afrika," alisema Kamwe.

Aliongeza kwa sasa wanatarajia kupata wageni wengi kutoka mataifa mbalimbali huku CAF pekee ikileta maofisa wake zaidi ya 200.

"Sasa twende zetu Algeria na lengo kubwa kutafuta mashabiki kwenda nao na utaratibu ni ule ule wa awali wa kucheza bahati nasibu ili kupata nafasi ya kwenda nchini humo," alisema msemaji huyo.

Naye Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki wa Yanga, Haji Mfikirwa, alisema huu ni wakati mahususi kwa mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kujitokeza kwa wingi uwanjani kuishangilia timu yao.

Mfikirwa alisema wamepokea tiketi nyingi tofauti na awali ambazo walikuwa wanapata katika michezo ya nyuma walipokuwa wakifanya harambee.

"Hadi sasa tumepokea jumla ya tiketi 18,213 kutoka kwa wadau mbalimbali akiwamo Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu, na tumeanza mchakato wa kuzigawa kwa wanafunzi wa vyuo na nyingine tunasubiri utaratibu mwingine wa kuwafikia wanachama wetu na mashabiki," alisema Mfikirwa.



Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Jamhuri, Jayden Frank (kulia), akimiliki mpira dhidi ya mwenzake, Binoy Richard, wakati wakifanya mazoezi kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Simba yanasa bosi wa usajili

INATOKA UK 24

Wakati huo huo taarifa zaidi kutoka Simba zinasema wanajipanga kuibomoa Vipers kwa kuwanasa waliokuwa wasaidizi wa Robertinho alipokuwa akiifundisha klabu hiyo ya Uganda.

Katika hatua nyingine, hatima ya kiungo, Hassan Dilunga, ambaye amerejea kwenye mazoezi ya kikosi cha Simba bado haijajulikana.

Dilunga ambaye aliwahi kuonekana akifanya mazoezi na JKT Tanzania iliyorejea kwenye Ligi Kuu Bara, anawindwa pia na Mtibwa Sugar.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema mchezaji huyo alikuwa chini ya uangalizi wa madaktari na makocha kwa miezi miwili kwa ajili ya kumwangalia utimamu wake wa mwili pamoja na maeneo ya majereha yake.

Alisema Simba ilikosa moja ya wachezaji wa aina ya Dilunga msimu huu ambaye ana uwezo wa kucheza kama winga, kiungo mzuiaji, kiungo wa kati na hata namba 10, hivyo kama atakuwa na kiwango chake kile kile basi atakuwa msaada mkubwa kwenye kikosi.

# Michezo

Nipashe

Ijumaa Mei 26, 2023



Southgate aamua kumtema Sterling UK. 21




Washiriki wa Warsha ya Mafunzo ya Leseni ya Klabu yaliyoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) wakiwa katika picha ya pamoja kwenye hoteli ya Johari Rotana, Dar es Salaam. Warsha hiyo iliyoshirikisha viongozi kutoka nchi 17 za Afrika ilimalizika jijini jana. **PICHA: TFF**

# YANGA HATARI ZAIDI NDANI YA BOKSI CAF

## Mayele, Musonda wakali wa kupachika na ku-assist, yafunga 2 kwa vichwa huku...

**Na Adam Fungamwango**

KWA sasa ni Yanga pekee ndio inasubiriwa kutimiza ndoto ya kuwa klabu ya kwanza Tanzania kuleta Kombe la Afrika.

Hata hivyo wakati ikijiandaa na mechi hiyo ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kuwakaribisha USM Alger kutoka Algeria, takwimu zinaonyesha mabao yao mengi wameyafunga ndani ya eneo la hatari, huku mastraika wao waliofunga mabao mengi kwenye michuano hiyo, Fiston Mayele na Kennedy Musonda pia wanaongoza kwa kutoa pasi za mwisho 'asisst.'

**Takwimu za Yanga katika michuano hiyo zinaonyesha kati ya mabao 15 waliyofunga, mechi 10 ilizocheza tangu hatua za makundi, mabao 13 yamefungwa ndani ya eneo la hatari.**

Ni mabao mawili pekee ambayo yamefungwa nje ya boksi, nayo ni lile alilofunga kiungo, Mudathir Yahaya Februari 19, mwaka huu walipocheza dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na kushinda 3-1 hapa Dar es Salaam.

Bao lingine la nje ya 18 lilifungwa na Mayele kwenye mechi dhidi ya Real Bamako ugenini Februari 26, mwaka huu huku timu hizo zikitoka sare goli 1-1.

Yanga inaonyesha haifungi sana mabao yake kwa vichwa, kwani ni mawili tu ambayo yamepachikwa kwa njia hiyo na mfungaji ni mmoja tu, Musonda.

Alifunga bao kwa njia hiyo kwenye mechi dhidi ya TP Mazembe hapa nyumbani na lingine akilifunga kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya US Monastir ya Tunisia, waking'ara kwa ushindi wa mabao 2-0.

Kati ya mabao 15 ya Yanga, 11 yamefungwa kwa mguu wa kulia, na manne kwa mguu wa kushoto.

Mabao ya mguu wa kushoto ya Yanga yalianza kufungwa na Mayele ugenini Yanga ikicheza dhidi ya Real Bamako katika sare ya bao 1-1, Stephane Aziz Ki akifanya hivyo timu yake ilipocheza dhidi ya Marumo Gallants Mei 10, mwaka huu nyumbani na kushinda mabao 2-0, Bernard Morrison akifunga bao kwa mguu wa kushoto kwenye mechi hiyo hiyo na Musonda akipachika bao, wakati wa mechi ya mkondo wa pili ya nusu fainali iliyochezwa Afrika Kusini, Yanga ilishinda mabao 2-1.

Takwimu zinaonyesha viungo wa Yanga hawatengenezi sana nafasi za kufunga, mastraika wao tegemeo, ndiyo wanaongoza kwa pasi za mwisho.

Kiungo pekee aliyetoa pasi ya mwisho ni Aziz Ki, akimlisha Mayele kwenye mechi ya ugenini dhidi ya Real Bamako.

Musonda ndiye kinara wa 'assist' kwenye timu hiyo, mechi za kimataifa akiwa ametoa pasi za mwisho nne, lakini pia akifunga mabao matatu mpaka sasa, hivyo kuchangia jumla ya mabao saba.

Mayele, mwenye mabao sita mpaka sasa anayeongoza katika ufungaji si kwa Yanga tu bali michuano yote, anashika nafasi ya pili kutoa pasi za mwisho, akiwa na 'assist' tatu, na kuchagia mabao tisa, na anayeshika nafasi ya tatu ni beki, nahodha wa timu hiyo, Bakari Mwamnyeto akiwa nazo mbili.

Mwamnyeto ni mchezaji pekee ya kizawa aliyetoa 'assist' kwenye michuano hiyo, nayo alizipata walipokuwa Nigeria kucheza dhidi ya Rivers United na kushinda mabao 2-0, ambapo alikuwa na kazi ya kumwekea Mayele na kutumbukiza wavuni.

Wengine waliotoa 'assist' ni Djuma Shaaban, Aziz Ki, Jesus Moloko na Tuisila Kisinda.

Hiyo inafikisha jumla ya wachezaji saba, waliochangia mabao mpaka sasa kwenye mechi 10 ilizocheza Yanga hadi kufikia mechi ya kwanza ya fainali itakayopigwa keshokutwa.

## Simba yanasa bosi wa usajili

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umemtambulisha rasmi, Mels Daalder, raia wa Uholanzi kuwa 'Skauti Mkuu' wa timu hiyo kwa ajili ya kusimamia mchakato wa kusaka nyota wenye vipaji kutoka sehemu mbalimbali duniani, imefahamika.

Uamuzi huo wa Wekundu wa Msimbazi unalenga kuimarisha kikosi chao kuelekea msimu ujao wa mashindano kwa ajili ya kufanya usajili wa wachezaji wenye viwango bora.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Mtandaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema eneo la skauti ya wachezaji ni muhimu ingawa lilikuwa haipewi nafasi kubwa miaka ya nyuma na klabu yao imeamua kwenda kisasa kwa kumwajiri Mels.

Kajula alisema mtaalum huyo atashirikiana vizuri na Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' katika kufanya usajili kulingana na 'mapinduzi' anayotaka kuyafanya mwalimu huyo.

"Tunafuraha kubwa kumkaribisha Mels ili kuja kuboresha ufanisi kwenye Skauti kwa sababu ni eneo muhimu katika mafanikio ya klabu yetu.

Tunaendelea na maboresho muhimu kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa," alisema Kajula.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002